

**GUARDIOLA: NIMEFUNGA UKURASA WA CITY 2023**

UKURASA 21

**Chuo** chatoa tamko kuhusu udahili wa Nape



UKURASA 3

**Waziri** akiri ajira vijana bado tatizo

UKURASA 3



**Tshisekedi** aongoza matokeo awali DRC

UKURASA 17


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 24, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • No. 0581534

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Waziri Silaa ageukia ujenzi vituo mafuta

• **Apiga** 'stop' huduma kituo kimoja, adai walitaka kumhonga mil. 300/- *Ukurasa 2*



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, akizungumza wakati akisimamisha huduma kituo cha mafuta cha Barrel, Mikocheni, Dar es Salaam na kupiga marufuku ujenzi holela wa vituo katika makazi ya watu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## MAKALA MAALUM

# Kikongwe amwangukia Samia madai ya serikali kumpoka shamba

UK. 4



# Kigogo wa UDART jela miaka mitatu, faini mil. 200/-

UKURASA 2

**MICHEZO** **STARS KWENDA MAWINDONI ALGERIA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Mkurugenzi UDART na wenzake jela miaka mitatu, faini mil. 200/-

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imewatia hatiani na kuwahukumu kifungo na kulipa faini jumla ya Sh. milioni 200 aliyekuwa Mkurugenzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (UDART), Robert Kisena na wenzake wawili.

Mahakama hiyo imewatia hatiani washtakiwa watatu na kumwachia huru mmoja juzi mbele ya Jaji Elinaza Luvanda, baada ya kujiridhisha kwamba mashtaka dhidi yao yamethibitishwa.

Waliotiwa hatiani mbali na Kisena, ni Mkurugenzi wa UDA, Charles Newe na Mtunza Fedha wa UDART, Tumaini Kulwa. Pia mahakama ilimwachia huru mfanyabiashara John Samangu, baada ya kuona hakuna ushahidi wa kuthibitisha mashtaka dhidi yake.

Washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na mashtaka 15 yakiwamo kuisababishia UDART hasara ya Sh. milioni 750, kuongoza genge la uhalifu, utakatishaji fedha haramu, kuwasilisha nyaraka za uongo na kughushi.

Katika shtaka la kuongoza genge la uhalifu, washtakiwa wanadaiwa katika nyakati tofauti kati ya Mei 25 na Julai 10, 2016 katika maeneo tofauti Dar es Salaam, waliongoza genge la uhalifu na kujipatia Sh. milioni 750 kutoka akaunti ya UDART, Benki ya NMB Tawi la Bank House.

Washtakiwa hao pia walikuwa wanakabiliwa na mashtaka mawili ya kughushi, mawili ya kuwasilisha nyaraka za uongo na mashtaka tisa ya utakatishaji fedha haramu.

Katika mashtaka ya kughushi ilidaiwa kuwa Mei 26, 2016, Dar es Salaam, kwa udanganyifu na kwa makusudi, walighushi fomu ya kuhamisha fedha wakionyesha UDART imehamisha Sh. milioni 750 kutoka katika akaunti yake iliyoko Benki ya NMB kwenda akaunti inayomilikiwa na Kampuni ya Longway Engineering Ltd iliyoko Benki ya KCB za ujenzi wa vituo vya mabasi na uzio Kimara, Kivukoni, Ubungo na Morocco, wakati wakijua si kweli. Katika ushahidi inadaiwa Sh. milioni 260 zilihamishiwa katika akaunti ya Universal Cargo Trans-Shipment Holding Ltd, Sh. milioni 204 zilihamishiwa kwa mshtakiwa wa kwanza na watatu.

Aidha, Sh. milioni 36 zilihamishiwa kwa TaonKang, Sh. 79,780,000 zilihamishiwa kwa mshtakiwa wanne na jumla ya Sh. 9,535,000 zilitolewa kutoka katika akaunti ya Universal Cargo. Kwa kufanya hivyo, washtakiwa walisababisha hasara ya Sh. milioni 750 kwa USA.

Katika shauri hilo upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi 24 na vielelezo 60 huku upande wa mashtaka ukiwakilishwa na Wakili wa Serikali, Dickson Shayo, na Blandina Mnung'a.

Upande wa utetezi uliwakilishwa na Wakili Nduruma Majembe, Deusdedit Luteja, Doreen Karugila na Wakili Habibu Kassim.

Mahakama baada ya kupitia ushahidi na utetezi wa washtakiwa ilibaini kwamba, hakukuwa na ushahidi dhahiri wa kuthibitisha kwamba mshtakiwa wa kwanza, pili na mshtakiwa watatu waliidhinisha Sh. milioni 750.

"Kwa kuzingatia hoja ya hapo juu, mahakama inamwachia huru mshtakiwa wa tatu kwa shtaka namba moja na 15 pia.

"Hakuna chochote katika kumbukumbu kinachothibitisha kwamba alishiriki katika njama hiyo ya uhalifu au alifanya kitendo chochote cha makusudi kusababisha hasara,"alisema Jaji Luvanda.

Alisema upande wa mashtaka umethibitisha mashtaka dhidi ya mshtakiwa 1, 2 na 4, hivyo mahakama inawatia hatiani kwa makosa waliyoshtakiwa nayo.

Baada ya kutiwa hatiani upande wa utetezi uliomba wateja wao wapunguziwe adhabu kwa sababu ni wakosaji wa mara ya kwanza huku upande wa Jamhuri ukiomba wapewe adhabu kwa mujibu wa sheria ili iwe fundisho.Akitoa adhabu alisema mahakama inazingatia hoja kwamba washtakiwa ni wakosa wa mara ya kwanza.

"Kosa la kwanza mshtakiwa 1,2 kila mmoja atakwenda jela miaka mitatu, kosa la pili mshtakiwa 1,2 watakwenda jela miaka mitatu, kosa la tatu mshtakiwa wanne atakwenda jela miaka mitatu.

"Kosa la 6,11 na 12 mshtakiwa 1,2 wanahukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 100 wakishindwa watakwenda jela miaka mitano, kosa la 13 na 14 mshtakiwa 1,2,4 wanahukumiwa kulipa faini Sh. milioni 100 wakishindwa watakwenda jela miaka mitano na kosa la 15 mshtakiwa 1,2 na 4 watakwenda jela miaka mitatu,"alisema.

Jaji Luvanda alisema adhabu hizo zinakwenda kwa pamoja. Kutokana na hali hiyo, alisema washtakiwa wakilipa faini ya Sh. milioni 200 watatumikia kifungo cha miaka mitatu, endapo watashindwa kulipa faini watatumikia kifungo cha miaka mitano.



Eneo la barabara likiwa na shimo na kuwekwa alama ya tairi la gari ikiwa ni alama ya tahadhari kwa madereva wanaotumia barabara hiyo juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Silaa ageukia ujenzi vituo mafuta

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amegeukia ujenzi holela vituo vya mafuta kwa kusimamisha matumizi ya kituo kampuni ya Barrel Petrol Energy, kilichoko Mikocheni, Dar es Salaam.

Ameagiza vituo vyote vilivyojengwa katika makazi ya watu nchini kote kusimamishwa mara moja huku akibainisha kuwa amekataa rushwa ya Sh. milioni 300.

"Kwa mamlaka niliyopewa na sheria ya Bunge, ninasimamisha matumizi ya kituo cha mafuta eneo hili na maeneo mengine kwa sasa na eneo la Msasani. Nitaangalia namna ya kupata timu ya watu waadilifu ili wakija hapa (kituo cha mafuta) wataona sura ya jambo hili lilivyofanyika.

"Pili, ninawaagiza wakuu wa idara ya ardhi na mipango miji kufanya uhakiki wa vituo vyao vya mafuta, kwa maana mchakato uliotumika, ukubwa wa viwanja, ukaribu wa kituo kimoja na kingine na ukaribu wa maeneo mengine ya kutolea huduma za jamii, hali ya uendelezaji na kuwasilisha ofisini kwangu Januari 31, 2024," alisema.

Silaa ambaye jana alikwenda kituoni hapo akiwa ameambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kinondoni, baada ya ukaguzi katika eneo hilo, alitoa maagizo mbalimbali.

"Mimi si mtaalam wa rushwa na kunapokuwa na rushwa kila kitu hukuoni. Utaona kila kitu kipo sahihi. Hawa wazee, hawa wananchi utawaona hawana maana, kuweka zege utaona ni sawa.

"Hiki kituo ninakijua si kwa kukiona kwa kukisikia, wakati ninatoa maagizo ya ujenzi holela ya vituo, wananchi wanaokaa hapa wengi walinipigia simu wakaniambia wewe mbona unahangaika mikoani wakati Mikocheni kuna kituo kinajengwa kwa kasi sana labda wanakimbizana na agizo lako. Niliwaambia hakuna haraka kwenye sheria nitapata nafasi nitakuja," alisema.

Waziri Silaa alisema alipomwona Anna Tibaijuka (akizungumza katika video fupi akitoa malalamiko ya kituo hicho hivi karibuni), alidhani anakaa Makongo, hivyo aliwatumia video hiyo wataalamu wake kwa ajili ya ufuatiliaji.

Alisema baada ya ziara zake mikoani, kuna mtu alimwuliza kama ameona hiyo video fupi ya Tibaijuka na kukiri aliiona lakini hajaifanyia kazi.

"Huyo mtu ni rafiki yangu, ametumiwa video hiyo na rafiki yangu mwingine, akaniambia wanakutafuta wenye kituo'. Kwa hiyo wamemtafuta rafiki yangu mmoja ili animudu, akamfuata anayenimudu akaniambia, 'Mheshimiwa Waziri pale kuna mia tatu yako.

"Yeye anasema mimi ninamjua yule mtu tutagombana, yeye hafanyi hizo habari. Ndio ananihadithia akanifanya nirudi kwenye ile video fupi kujua kipo wapi? Akaniambia kiko Mikocheni, nikamwambia ninakijua.

"Mimi si mtoto wa mkulima. Baba yangu alikuwa rubani, mpaka leo ninakula fedha za urithi. Baba yangu amefariki (dunia), mama yangu amefariki (dunia), bibi zangu wote wamefariki. Nina mke na mtoto mmoja.

Sinywi pombe wala sivuti sigara, hujawahi kuniona baa yoyote kwa hiyo Sh. 10,000 au Sh. 20,000 kwa siku inanitosha. Sijafikia kuhongwa milioni, ukiniambia Sh. milioni 300 ninaipeleka wapi?" alihoji.

Alisema mchakato huo wa kujengwa kituo eneo hilo haujafuata utaratibu na tayari juzi amemsimamisha mkurugenzi.

"Niwaambie Watanzania mtu akikwambia kuna fedha ya Waziri ng'ang'ania ukamwone mwenyewe ila kazi hiyo sifanyi lakini kuna watu wanaweza kukwambia 'nipe nitamfikishia DC (Mkuu wa Wilaya). "Jana (juzi) usiku nilikuwa nimezima simu nilipowasha nikaona mnanitafuta tena mwambie tajiri kama ana fedha zinamsumbua kuna msikiti wa Ujumaa pale Gongo la Mboto, mwambie akatafute dhawabu," alisema.

Waziri Silaa alisema Januari, mwakani, atakaa na wafanyabiashara wa mafuta ili wakubaliane kwa kuwa hawezi kukubali waharibu mji. Alisema kanuni ya mwaka 2018 ameisimamisha pamoja na mabadiliko ya matumizi ya ardhi nchi nzima.

Aliwaagiza wakuu wa idara za ardhi na mipango miji nchi nzima kufanya uhakiki wa vituo vya mafuta kwa maana viwanja, mabadiliko ya matumizi ya ardhi na itakapobidi kila mtu ashirikishwe na pia hakuna mabadiliko ya michoro ya mipango miji.

Kadhalika amewaagiza wafanyabiashara wa mafuta wakae mpaka Januari 31, mwakani, wafanye uhakiki wa vituo vyao, mchakato wa namna walivyobadilisha matumizi ya ardhi, vingapi viko karibu au makazi ya watu na kuwasilisha taarifa ofisini.

Mzee Stephen Rupia, ambaye ni mkazi wa eneo hilo, alisema hawakuona bango la kubadilisha matumizi ya eneo hilo kutoka makazi hadi kujengwa kituo hicho cha mafuta. Alisema wananchi wa eneo hilo hawakushirikishwa katika hatua yoyote.

Mhandisi Stanley Kitundu, akizungumza kwa niaba ya mmiliki wa kituo hicho, alisema wamepokea maelekezo hayo na watayatekeleza.

Alisema ujenzi wa kituo hicho umekamilika kwa asilimia 100 lakini bado hakijaanza kutoa huduma.

# HABARI KITAIFA

## Chuo Kikuu chatoa tamko udahili Nape

**Na Romana Mallya**

CHUO Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kimetoa ufafanuzi kuhusu mwanafunzi wake, Nape Nnauye, aliyedahiliwa chuoni hapo kwa masomo ya shahada ya kwanza ya sheria kwa mwaka wa masomo wa 2022/23.

Kwa mujibu wa taarifa ya chuo iliyotiwa saini na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Utafiti na Ushauri, Prof. Deus Ngaruko, ufafanuzi huo umetolewa baada ya hivi karibuni kuwapo taarifa zisizo sahihi zikisambaa katika mitandao ya kijamii kuhusu udahili wa Nape.

Prof. Ngaruko alisema Nape amedahiliwa kwa vigezo na sifa timilifu kama zilivyoainishwa kwenye prospectus ya chuo ya mwaka 2022/23. Pia alisema ana sifa hizo kwa mujibu wa kitabu ukurasa wa 8-9 ambapo sifa namba tatu katika kitabu hicho ndiyo iliyotumika kumdahili mtajwa.

"Miongozo hiyo ya udahili inapatikana kupitia www.out.ac.tz na www.tcu.go.tz. Nape ni mwanafunzi halali wa Chuo Kikuu Huria Tanzania ambaye amedahiliwa kwa kukidhi vigezo vyote stahiki," alisema. Taarifa hiyo ilisema OUT imeanzishwa kwa Sheria ya Bunge namba 17 ya mwaka 1992, kwa malengo ya kuongeza fursa za elimu ya juu kupitia mifumo ya kutoa elimu kwa njia ya masafa.

"Huria ni mtandao kwa watu wote ambao wanapenda kujiendeleza kielimu na huku wanaendelea na kazi zao na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali, hivyo kuwa vigumu kwao kujiunga na vyuo vya bweni," alisema.

## Mnyeti awatangazia neema wauza samaki

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

NAIBU Waziri wa Mifungo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, amewaondoa hofu wafanyabiashara wa Soko Kuu la Samaki la Migombani lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kuwa, liko mbioni kufanyiwa ukarabati ili biashara kufanyika katika mazingira rafiki.

Mnyeti alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano mkuu wa kupokea taarifa ya utekelezaji miradi Jimbo la Sengerema ambapo alisema, serikali inatarajia kuanza utaratibu wa kukarabati soko hilo.

Alisema soko hilo ndilo linalosambaza samaki Kanda ya Ziwa hivyo lazima kuhakikisha miundombinu yake imekaa katika hali ya kuridhisha.

Pia alisema serikali itahakikisha inafanya ukarabati wa mabwawa ya Sengerema na kufufua mialo yote ambayo kwa sasa haitumiki kwa sababu ya kukosa miundombinu. Mnyeti aliwataka wavuvi kuacha uvuvi haramu badala yake watumie boti ambazo zinatolewa na serikali ili kusaidia kuondoa usumbufu wa kuingia ziwani na kuvua bila kuwa na uhakika wa kupata samaki.

Mbunge wa Sengerema, Tabasamu Mwangao, aliiomba serikali ikamilishe miradi ambayo imeanzishwa ikiwamo ya elimu iliyoanzishwa na kusubiri ukamilishwaji. Kuhusu soko hilo, Tabasamu alisema endapo litafanyiwa maboresho vijana wanatachangamkia fursa ya kusambaza samaki na kujiinua kiuchumi.




Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa kwenye picha ya pamoja na wadhamini wa tuzo za Rais kwa wazalishaji bora nchini (PMAYA), zilizoandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) zilizofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Wa pili kushoto waliosimama ni Mkuu wa Mawasiliano wa SBC Tanzania Limited Foti Gwebe Nyirenda. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri akiri ukosefu ajira tatizo

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amesema tatizo la ajira nchini bado ni kubwa na linaipasua kichwa serikali.

Kutokana na hali hiyo, amesema mkakati mkubwa wa serikali kwa sasa ni kutengeneza ajira mpya kwa Watanzania wanaohitimu kwenye vyuo vikuu mbalimbali nchini ili wapate kipato cha kuwawezesha kuondokana na umaskini.

"Kutokuwa na ajira ni hatari lakini hatari zaidi ni pale unapokuwa na vijana wengi wamemaliza vyuo vikuu na hawana ajira, hii inakuwa shida sana. Kwa hiyo kutengeneza ajira ni ajenda yetu muhimu sana,' alisema

Moja ya mikakati hiyo ni kwamba serikali inaweka mipango kuhakikisha kunakuwa na ongezeko kubwa la mauzo ya nje ya nchi kwa bidhaa ambazo zimeongezewa thamani nchini badala ya kupeleka malighafi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Bodi ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na kuwapa maagizo na malengo wanayotakiwa kufikia kuhusu kuvutia uwekezaji.

Prof. Mkumbo alisema lengo kubwa la serikali kwa sasa ni kuongeza mauzo ya nje kama njia ya kukuza pato la taifa. Aliongeza kuwa miaka 20 iliyopita serikali imekuwa ikijitahidi kuongeza mauzo ya nje kutoka chini ya dola bilioni moja hadi dola bilioni sita kwa mwaka.

"Ni kweli tumeongeza mauzo ya nje lakini changamoto kubwa ni kwamba tumeuza bidhaa nyingi zikiwa ghafi kwenye madini, kilimo, uvuvi, kwa hiyo tunataka kuona bidhaa hizo zinaongezewa thaamani hapahapa nchini, utaratibu wa kuuza malighafi lazima tuachane nao," alisema

Waziri Mkumbo pia alisema lengo lingine la serikali ni kuhakikisha shughuli za uzalishaji mali zinafanyika kote nchini kwa kutumia nishati ambayo haichafui mazingira ya Tanzania na duniani kama maazimio mbalimbali duniani yanavyotaka kuhusu hewa ukaa.

Alisema Tanzania inataka kuona uchumi unakuwa jumuishi, unaozalisha ajira nyingi na ambao unaongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi na unaoleta ustawi kwa wananchi wote badala ya kunufaisha wachache.

"Tunataka kuona uchumi unakuwa lakini uwe uchumi jumuishi unaosaidia wananchi wengi kwa sababu uchumi unaweza kukua lakini ukasaidia watu wachache.

Nawaabia haya kwa sababu mnapoweka mikakati ya kuvutia wawekezaji ni lazima mjue malengo ya serikali ni yapi ndipo myatekeleze.

"Serikali inahitaji uchumi mpya unaoendana na idadi ya watu kwa sababu mkibaki na uchumi ule ule hamwezi kuongeza wigo wa kukusanya kodi wala pato la taifa haliwezi kuongezeka. Ili pato la taifa liongezeke, tunahitaji uwekezaji mpya na kodi mpya," alisema.

Prof. Mkumbo alisema takwimu zinaonyesha kuwa wawekezaji wengi wanapendelea kuwekeza kwenye sekta ya uzalishaji viwandani, kilimo, majengo ya biashara na usafirishaji, hivyo kuitaka TIC kuendelea kuvutia wawekezaji kwenye maeneo mbalimbali.

Aliwataka Watanzania kuendelea kuchangamkia fursa za uwekezaji na kuachana na dhana kwamba serikali inapozungumzia uwekezaji inakuwa inazungumzia wageni.

"Taarifa za robo mwaka zilizotolewa na TIC zimeonyesha kwamba watanzania wanazidi kuchangamkia fursa za uwekezaji na juzi tulifungua mauzo ya hatifungani za NMB asilimia 99 ya walionunua ni watanzania nawapongeza sana tusidhani uwekezaji ni kwaajili ya wageni peke yao nasisi tunahusika," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya TIC, Dk. Binilith Mahenge, alimpongeza Waziri Mkumbo kwa kusimamia mikakati mbalimbali ya kuinua sekta ya uwekezaji kwa lengo la kuinua pato la taifa na kuongeza ajira kwa watanzania.

"Nikuhakikishie Waziri yale uliyotuelekeza tutayafanya ndani ya muda mfupi hatutasubiri tutaanda mikakati ya kuendelea kuijenga taasisi hii na kuvutia idadi kubwa ya wawekezaji mwaka hadi mwaka," alisema Dk. Mahenge.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...28/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: KOPILATO SHABALA MDIE wa SOKOINE KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA DANIELY KOPILATO**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 28 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 22 mwezi 12 mwaka 2023

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO.26751 OF 2023**

**IN the Matter of the late:ROSE PAUL MTALI**

**By 1.LEILA FABIAN MTALI**
**2.............................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 14th day of January 2024.

Dated at ............ this 12 day of DEC 2023.

RESIDENT MAGISTRATE

MAKALA MAALUM

# Kikongwe amwangukia Samia mgogoro wa shamba na kijiji

**Na Thobias Mwanakatwe, aliyekuwa** KOROGWE

KIKONGWE Zaina Kipanga (88), mkazi wa Kijiji cha Kwakombo, Kata ya Kwakombo, Korogwe mkoani Tanga, amemwangukia Rais Samia Suluhu Hassan, kuhusu mgogoro wa shamba ekari 12 baina yake na serikali ya kijiji cha Kwamsisi, Korogwe mkoani Tanga.

Zaina amedai kuwa serikali ya kijiji chicho, imefyeka mazao ya mahindi aliyoyapanda msimu huu katika shamba hilo kutokana na mgogoro baina yake na kijiji hicho.

"Ninamuomba Rais Samia aingilie kati ili nipate haki yangu, Serikali ya Kijiji cha Kwamsisi imefyeka mahindi katika shamba langu hili," alisema.

Licha ya viongozi wa wilaya ya Korogwe kufahamu mgogoro huo, alisema wameshindwa kumsaidia hali aliyoiita ni njama za makusudi za kutaka kumdhulumu shamba hilo lenye ekari 12.

Kikongwe huyo alisema amelazimika kumwomba Rais Samia amsaidie kwa kuwa hajui hatima ya maisha yake, kwa kuwa hana chakula wala shamba baada ya serikali ya kijiji hicho kumnyang'anya ardhi hiyo.

Alisema shamba hilo ambalo sasa amepigwa marufuku kuingia, yeye na mumewe, Waziri Kipanga, ambaye sasa ni marehemu, walikuwa wakilima tangu wakati wa operesheni vijiji iliyofanyika miaka ya 1970.

Kikongwe huyo alisema viongozi hao wamekusudia kuwanyang'anya shamba hilo ambalo ndani yake kuna makaburi ya familia kwa kuwa lina mazao ya kudumu kama miembe, minazi na miti aina ya mitiki.

Alisema kabla ya mume wake kufariki dunia, wakiwa nyumbani kwao na mke mwenzake, walifika watu na kuwaambia kuwa wamepita kwenye eneo la shamba hilo na wamekuta kumsagari na watu wanajenga nyumba na walipofuatilia walibaini taarifa hizo ni za kweli.

Alisema walipohoji waliambiwa kuwa kuna mradi wa ufugaji wa ng' ombe wa maziwa unatarajiwa kuanzishwa hapo bila kuambiwa aliyetoa idhini kupisha mradi huo.

Kwa mujibu wa kikongwe huyo, mradi huo haukuendelea mpaka majengo yaliyojengwa shambani hapo yalipobomoka na wao waliendelea na shughuli za kilimo hadi serikali ya kijiji ilipoibuka na kudai shamba hilo ni mali yake.

Alisema licha ya suala hilo kufikishwa katika vyombo mbalimbali vya sheria, serikali ya kijiji hicho imeshindwa kuthibitisha uhalali wa kudai shamba hilo ni mali yake halali.

Kikongwe huyo alisema ekari 12 ziko ndani ya ekari nyingine 38 ambazo mradi huo ulikuwa ufanyike, lakini ziliuzwa na watu waliokuwa wakilima.

"Cha kushangaza waliouza wapo na wala hawajachukua hatua yoyote jambo ambalo linaonyesha kuna hila inafanyika," alisema .

Watoto wa bibi huyo, Said Kipanga, Mariam Kipanga, Mkiwa Kipanga na Abdallah Kipanga ambao sasa ni watu wazima, wanasema wazazi walikuwa wakiishi katika eneo hilo na wanashangaa kuona serikali ya kijiji ikiwafukuza.

Msimamizi wa miradhi wa familia hiyo, Said Kipanga, alisema amepata misukosuko mingi ikiwamo kuwekwa mahabusu mara kwa mara kutokana na kufuatilia jambo hilo.



Zaina Kipanga (88) akiwa katika huzuni wakati akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni.



Zaina Kipanga akiwa na watoto wake, Mariam (kushoto) na Mkiwa (katikati) wakati wakizungumza na waandishi wa habari

Alisema licha ya kuwekwa tangazo la mirathi kwa muda wa miezi mitatu kuhusu mali za baba yao likiwamo shamba hilo, hakuna mtu yeyote aliyejitokeza kupinga, hivyo wanashangaa serikali ya kijiji kuanza kujitokeza hivi sasa kudai ni ardhi yake.

**MASHUHUDA WANENA**

Mkazi wa kijiji hicho, Hemed Mwigole, ambaye ni jirani katika eneo hilo linalodaiwa kuwa ni la mradi, alisema familia hiyo haitendewi haki kwa kuwa mashamba hayo yalikuwa ya wazazi wao tangu wakati wa operesheni vijiji.

Mwenyekiti mstaafu wa kijiji hicho, Hamadi Mwinyimsanga aliyeshika madaraka mwaka 1983 hadi 2006, alisema wakati wa uongozi wake hakukuwapo na chokochoko hizo wala kuona vielelezo vyovyote vinavyoonyesha uhalali wa kijiji kumiliki shamba hilo.

"Wakati wa uongozi wetu kwa kuzingatia shamba hilo lilikuwa likitumiwa na familia hiyo tangu wakati wa operesheni vijiji na baada ya kuona hakuna mradi unaoendelea katika eneo hilo licha ya kujengwa miundombinu kama josho na mabanda, tuliridhia familia hiyo kuendelea kulima shamba hilo lenye ekari zaidi ya 15 hivi," alisema Mwinyimsanga.

Alibainisha kuwa mradi huo haukufanikiwa kutokana na kutokidhi vigezo na hata kwenye ramani ya kijiji hicho hakuna sehemu inayoonyesha kuwapo kwa suala hilo, hivyo baada ya hapo, kila mtu aliyekuwa na shamba lake kwenye eneo hilo aliendelea kulima huku wengine wakiyauza.

Mwinyimsanga alisema tangu mwaka 1972 hadi alipostaafu mwaka 2006, hakukuwapo na changamoto yoyote kuhusu shamba hilo na hata viongozi wengine waliofuatia waliendelea kuiachia familia hiyo kuendelea kulitumia.

Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji hicho, Salehe Msisi, akizungumzia suala hilo, alisema wakati anaingia madarakani alikabidhiwa eneo hilo na viongozi waliomtangulia likiwa na miundombinu ya josho na baadhi ya mabanda.

Alisema walimweleza kuwa shamba hilo ni mali ya serikali lakini hakuelezwa kama kijiji hicho kina hati ya umiliki wa eneo hilo.

Kuhusu madai ya kufyekwa kwa mazao ya familia hiyo, alisema wamekuwa wakilifanyia usafi lakini hajawahi kupata taarifa yoyote ya mazao kufyekwa.

**KAULI YA DED**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe, Tito Mganwa, akizungumzia kuhusu mgogoro huo, alikiri kuufahamu na kusema eneo hilo ni mali ya halmashauri hiyo.

Alisema awali shamba hilo lilikuwa likimilikiwa na serikali ya kijiji cha Kwamsisi na lilikuwa na miundombinu ya mifugo kama josho na nyumba ya watumishi.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kuna ekari kama 50 ambazo halmashauri imetenga kwa ajili ya kuanzisha mnada kwa ajili ya kuendeleza uchumi wa wananchi wa kijiji hicho na tayari wametenga fedha na katika mwaka wa fedha wa 2023/24, wanatarajia kujenga miundombinu kwa ajili ya kuanza rasmi mnada huo.



Watoto wa Zaina Kipanga, Mariam na Mkiwa wakikusanya mabaki ya mahindi yanayodaiwa kufyekwa na viongozi wa serikali ya kijiji cha Kwamsisi.
**PICHA ZOTE: THOBIAS MWANAKATWE**

## HABARI KITAIFA

# Kampuni yashiriki usafi kuunga mkono utunzaji wa mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Simu ya Halotel na wafanyakazi wake wameshiriki katika usafi ikiwa ni sehemu ya kusheherekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

Imesema imeshiriki usafi huo kwa kushirikiana na Ofisi ya Diwani wa Kijitonyama kusafisha Soko la Makumbusho katika kuunga mkono jitihada za kuliweka Jiji la Dar es Salaam katika hali ya usafi.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ambaye alishiriki katika shughuli hiyo, alisema amefurahishwa na kitendo cha kampuni hiyo kujali mazingira.

"Ninayo furaha kuona wadau mbalimbali kama Halotel wakiunga mkono jitihada za ustawi wa jamii katika sekta ya afya ambayo ndiyo muhimili wa maendeleo ya sekta nyingine katika Jiji la Dar es Salaam," alisema.

Mkurugenzi wa Sekta ya Biashara Halotel, Abdallah Salum, alisema katika kuhakikisha wanasaidia jamii na kuunga mkono harakati za upambanaji wamefanya usafi sokoni hapo.

Pia alisema wametoa vifaa vya usafi vitakavyowasaidia kuweka mazingira yao ya biashara katika hali ya usafi.

"Tunatambua changamoto mbalimbali zinazoikumba sehemu kama hii ya soko lenye mkusanyiko mkubwa wa watu.

"Kukiwa na vifaa vya kukusanya na kuhifadhia taka kama mafagio, reki na vihifadhia taka kutapunguza kuzagaa hovyo kwa taka katika eneo la soko," alisema.

Mmoja wa wafanyabiashara sokoni hapo, alisema, "Tunajisikia furaha sana Halotel kuja hapa na kushiriki nasi moja kwa moja kufanya usafi na kutuletea vifaa vya usafi katika soko letu.

Alisema usafishaji wa mazingira si jambo dogo na kilichofanyika kinahamasisha kuendelea kuyatunza mazingira.

Uongozi wa soko hilo umeishukuru Halotel kwa kuthamini afya za wananchi na kuunga mkono jitihada za kuisaidia sekta ya afya.

Halotel inaendelea kupiga hatua kubwa katika kusambaza huduma za mawasiliano na kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu nchi nzima, kampuni hii inaendelea kujihusisha na kutoa misaada mbalimbali kwa jamii ya Watanzania ikiwamo kuboresha sekta ya afya na elimu kama moja ya kipaumbele cha kampuni ya Halotel.




Gari la kubeba wanafunzi likiwa linapita kwenye dimbwi lililojaa maji mengi huku likiwa limebeba abiria wa kawaida katika eneo la Chanika Zingiziwa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Madereva wanaovunja sheria kunyang'anywa leseni

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MKUU wa Kikosi cha Usalama Barabarani Nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ramadhani Ng'anzi, amewataka abiria wanaosafiri kutoa taarifa za baadhi ya madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani ili hatua zichukuliwe.

Amesema madereva watakaokamatwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kunyang'anywa leseni.

Ng'anzi aliyasema hayo jana alipotembelea Kituo Kikuu cha Mabasi eneo la Shule ya Tanga, Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya ukaguzi wa vyombo vya moto mkoani hapa.

Akiwa kituoni hapo, Ng'anzi aliwaonya madereva wenye tabia ya ulevi na wanaoendesha mwendokasi kuwa wachukue tahadhari ili kulinda usalama wao, wa abiria na watumiaji wengine wa Barabara, wakiwamo watembea kwa miguu.

Pia alisema kwa madereva wanaosafiri umbali mrefu wahakikishe wanatii sheria za usalama barabarani na vileo ambavyo ndio chanzo cha ajali nyingi.

akishirikiana na askari wake, walikagua mifumo mbalimbali ya vidhibiti mwendo vya mabasi ikiwa ni pamoja na breki, matairi, ubora wa magari yenyewe pamoja na kuwapima madereva ulevi kabla ya kuruhusiwa kuanza safari.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Usafirishaji wa Mabasi ya Super Feo, Abdulab Kisiwa, alilishukuru Jeshi la Polisi kuona umuhimu wa kutembelea mkoani Ruvuma na kufanya ukaguzi huo.

Awali, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoani wa Ruvuma, Issa Milanzi, alisema ziara hizo ni mwendelezo wa kukagua vyombo vya moto na kuongea na madereva na abiria kama wanatumia tiketi za mfumo wa kierektroniki pamoja na kufunga mkanda wawapo safarini. Nao madereva wa mabasi walisema ujio wa kiongozi huyo kituoni hapo umewakumbusha umuhimu wa kufuata sheria za usalama barabarani ambazo ndizo huwaepusha na ajali.

## Uturuki yawatua kinamama ndoo

**Na Steven William,**
MUHEZA

TAASISI ya Silver Crescent kutoka Uturuki imetoa msaada wa kuchimba visima virefu vitano vya maji Muheza mkoani Tanga vinavyogharimu Sh. milioni 100 ili kusaidia wananchi kupata maji safi na salama bure.

Mratibu wa Taasisi hiyo Tanzania, Kadir Komurcu, alisema huo ni utaratibu wa kawaida kwao kusaidia jamii ili kuhakikisha inapata maji safi na salama.

"Tumekuwa na utaratibu wa kusaidia jamii hii ni muhimu kwa kuwa ina watoto, wazee na wenye ulemavu, hivyo tukiwasaidia haya maji wataweza kupunguza tatizo tunaamini na tuendelee kushirikiana," alisema.

Mratibu wa taasisi hiyo Mkoa wa Tanga, Omari Shariff, alisema visima hivyo vimechimbwa katika vijiji vya Sega, Lusanga, Genge, Mbaramo na Majengo.

Pia alisema wamepeleka madaktari bingwa katika kituo cha Afya cha Ubwari kwa ajili ya kutibu wananchi wa Muheza wanaosumbuliwa na ugonjwa wa mtoto wa jicho.

Alisema shughuli hiyo ya siku tatu imefunguliwa rasmi na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma.

Shariff alisema takribani wagonjwa 300 wamefanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho na kupewa miwani za jua ambapo zaidi ya milioni 36 zimetumika kutoa huduma hiyo.

Mkazi wa Kijiji cha Sega, Halima Juma, alisema kilichofanyika na taasisi hiyo kwa kuchimba visima hivyo ni sadaka tosha na wao kuondokana na changamoto ya maji.

Katibu Mwenezi mstaafu wa CCM, Wilaya ya Muheza, Makame Seif, ameishukuru taasisi hiyo ya Silver Crescent kwa msaada huo wa kuchimba visima vya maji na kutoa tiba bure ya macho kwa wananchi kwa kuwa wanamsaidia Rais Samia Suluhu.

Seif ambaye ni diwani mstaafu wa Kata ya Mbaramo, aliwaomba wadau hao kuendelea na moyo huo wa kusaidia jamii kwa maeneo mengine.

Silver Crescent yenye makao yake nchini Uturuki, imejikita kusaidia jamii katika upande wa kuchimba visima na kutoa matibabu bure ya macho na kutoa miwani za jua.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusherehekee siku ya Krismasi kwa amani, nidhamu na utulivu

**WAKRISTO** nchini, kesho wanaungana na waumini wenzao duniani kusherehekea Sikukuu ya Krismasi, ikiwa ni kusherehekea kuzaliwa kwa Mwokozi wao Yesu Kristo zaidi ya miaka 2000 iliyopita.

Pamoja na kwamba ni sikukuu inayowahusu Wakristo, kwa Tanzania ni siku ambayo huwaunganisha wananchi wote bila kujali imani zao katika kukusanyika, kula na kunywa pamoja. Hiyo yote ni kuonyesha kuwa Tanzania hakuna ubaguzi wa kiimani wala kiitikadi ndiyo maana kunapotokea sikukuu ya Imani nyingine, Wakristo nao hualikwa na kujumuika nao na kusherehekea.

Krismasi kama ilivyo ada kwa miaka yote, wako ambao husafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa ajili ya kuungana na ndugu zao ili kusherehekea. Ni wakati wa ndugu kukutana pamoja na kuzungumza masuala mbalimbali yakiwamo ya kimaisha na kifamilia na penye kasoro basi hutumia nafasi hiyo kuzirekebisha au kuzimaliza.

Aidha, waumini wa madhehebu mbalimbali ya Kikristo hukusanyika katika nyumba za ibada kwa ajili ya kushangilia kuzaliwa kwa Masihi wao. Ibada hizo huanza siku moja kabla ambazo hufanyika usiku kasha siku kama ya kesho ndipo husherehekewa kwa ibada kubwa ambazo hujumuisha waumini mbalimbali.

Kutokana na unyeti wa sikukuu hii, viongozi wa dini hasa maaskofu hutoa ujumbe mzito unaohusu jamii na nchi kwa ujumla. Kama kuna masuala ambayo yanaihusu nchi, viongozi hao hutoa matamko na kuishauri serikali kuyafanyia kazi. Miongoni mwa mambo ambayo yamekuwa yakikemewa ni rushwa, dekomrasia na kutaka serikali kuwajali wananchi. Katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, watu hujumuika katika sehemu za burudani kwa ajili ya kula na kunywa huku wengine wakienda kuburudika kwenye nyumba na maeneo yacstarehe. Baadhi ya vijana, watu wazima na watoto, huenda katika sehemu za ufukweni kwa ajili ya kuburudika.


Kwa ujumla, Krismasi ni sikukuu ambayo huambatana na matukio mbalimbali ya kiburudiani na ibada. Pamoja na kuwapo kwa matukio hayo, wako watu ambao hufanya mambo kupita kiasi hasa kwa kutumia vileo na wakati mwingine kusababisha matukio ya uvunjifu wa amani kama vile kupigana na kuumizana. Kwa maneno mengine, ni sikukuu ambayo huacha majanga kwa baadhi wanaoshindwa kujizuia na kufanya mambo ya ovyo. Baadhi ya watu hutumia vileo kupita kiasi na hata kushindwa kujitambua na kufanya mambo yasiyo ya staha katika jamii. Baadhi ya watu pia baada ya kupata vileo, huendesha magari kwa mwendo kasi na matokeo yake husababisha ajali ambazo huwafanya wapate majeraha au kupoteza maisha wao na watu wengine.

Krisimasi kwa Wakristo ni sikukuu kubwa ambayo maana yake ni kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu Kristo. Kabla ya sikukuu hii, kulikuwa na wiki nne za Maajilio ambazo hutumika kama sehemu ya waumini hao kutafakari juu ya maisha yao na kutengeneza mambo yao ambayo wanaona ni chukizo kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa mantiki hiyo, ni siku ambayo waumini wa Kikristo wanapaswa kuisherehekea kwa utulivu mkubwa na kutafakari kwa kina juu ya maisha yao yaliyopita. Kwa wale ambao wamemkosea Mungu, basi ni wakati wao wa kubadilika na kufuata mwenendo mzuri katika maisha anayoakisi Ukristo wa kweli. Sikukuu hii si ya kwanza na kutokana na uweli huo, Jeshi la Polisi nchini limeshatoa onyo kwa wote wanatakaofanya vitendo vya uvunjifu wa amani huku likiweka wazi kwamba limejipanga sawasawa kukabiliana na uhalifu huku likiwaonya watakaothubutu kwenda kinyume cha sheria kukiona cha mtema kuni.

Baadhi ya wazazi na walezi, wamekuwa wakitumia sikukuu kama hii kutembea nawatoto kwenda sehemu mbalimbali kwa ajili ya kufurahia. Kutokana na hali hiyo, jeshi hilo limewataka kuwa waangalifu na watoto wao pamoja na kuhakikisha usalama unakuwapo nyumbani kwa kuwa wale wenye nia ovu ya kuiba, hutumia mwanya huo kufanya vitendo hivyo. Ni vyema kila Mtanzania akatambua kwamba sikukuu kama hii si ya kufanya mambo ya ovyo na kwa Wakristo kuacha misingi ya Imani zao na kujiingiza katika ulevi na mambo yasiyompendeza Mwenyezi Mungu. Tusherehekee Krismasi kwa amani na utulivu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hongera serikali kuokoa asilimia 10 mapato ya halmashauri

**MWANZONI** mwa mwaka huu, serikali ilisitisha utoaji wa mkopo wa asilimia 10 unaotolewa na kila halmashauri kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, baada ya kubaini kuwapo kwa kasoro kadhaa.

Serikali ilifikia hatua hiyo hasa baada ya wabunge kulalamika kuhusu namna ya ukopeshaji wa mikopo hiyo, huku Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), ikidai kuwa fedha hizo zilikuwa zinaliwa na wajanja wachache na kusababisha walengwa kukosa.

Kamati hiyo ilijikita zaidi kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ambayo iliwahi kubainisha kasoro mbalimbali za ukopeshaji wa vikundi hewa mamilioni y

Ilikuwa Aprili 13 mwaka huu serikali ilipositisha utoaji wa mkopo huo, ili kuandaliwa utaratibu mzuri wa ukopeshaji wa fedha hizo kupitia benki, ili kuwasaidia zaidi wahitaji.

Hatimaye sasa serikali imekuja na utaratibu mpya wa utoaji mkopo huo ambao unatarajiwa kuanza kutumika rasmi Januari mwaka ujao, ili walengwa waweze kuupata bila usumbufu.

Akifungua Wiki ya Huduma ya Fedha Kitaifa, jijini Arusha hivi karibuni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anatoa maagizo kwa Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Fedha kumaliza mchakato wa utoaji wa mkopo huo uliokuwa umasitishwa.

Wito wa Waziri Mkuu katika mchakato huo, ni watoa huduma za fedha kuimarisha mifumo ya ukopeshaji na kutoweka vipengele vya mitego kwenye masharti ya mkopo na kwamba wananchi wanapaswa kuelewa masharti kabla hawajakopeshwa.

Niipongeze serikali kwa kuokoa fedha za walipa kodi kwa kuandaa utaratibu mpya wa ukopeshaji ambao ninaamini hautakuwa na vikwazo kama ilivyokuwa kwenye baadhi ya halmashauri.

Kimsingi, kelele zilikuwa nyingi kutoka kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambao walikuwa wanadai kuwa baadhi ya watumishi wa halmashauri walikuwa wakijikopesha wenyewe.

Si hayo tu wengine walikuwa wanadai kuwa wanafuatwa na kupewa masharti ya kupata mkopo huo, ikiwamo kukubali kuchukua sehemu ya mkopo na kuwapa watumishi waliowasaidia kuupata.

Aidha, wako walioamua kuachana na mkopo wa halmashauri, kwa kuwa walikuwa wakihangaishwa, huku watu wachache waliokubali masharti ya kutoa sehemu ya mkopo ndio wakawa wanapewa.

Changamoto za upatikanaji wa mikopo hiyo, zilisababisha baadhi ya wakopaji, hasa wanawake kuangukia kwenye mikopo umiza yenye masharti magumu ambayo ilikuwa imeshamiri kila mkoa.

Kupitia mikipo hiyo, wapo waliochukuliwa mali zao baadhi kushindwa kuirejesha kwa wakati na wengine kujikuta ndoa zao zikiwa ndani ya migogoro na nyingine kusambaratika.

Ninaamini kwamba, kwa utaratibu mpya ambao serikali imekuja nao kwenye mkopo wa asilimia 10 wa halmashauri, huenda ukawa ni mwarobaini kwa vikwazo ambavyo vilikuwapo ndani ya halmashauri.

Utaratibu huo unaweza kuwasaidia Watanzania kujikwamua kiuchumi kwani miaka ya nyuma waliachwa kama mbuzi asiye na mwenyewe na matokeo yake ikaibuka mikopo umiza kila kona na kuumiza kwelikweli.

Kwenye mikopo ya umiza, wapo baadhi ya wanawake awalioripotiwa kujinyonga, chanzo kikidaiwa kuwa ni kuzidiwa na madeni ya VICOBA na usumbufu kutoka kwa wanakikundi wenzao.

Kwa utaratibu ambao serikali imekuja nao wa kutoa mkopo ya asilimia 10 unaotokana na mapato ya ndani ya halmashauri, kwa kupitia benki, ni wazi imedhamiria kuwakomboa wanawake, vijana na walemavu.

kinachotakiwa ni kile ambacho Waziri Mkuu ameelekeza kwa watoa huduma za fedha kuimarisha mifumo ya ukopeshaji na kutoweka vipengele vya mitego kwenye masharti ya mkopo ili makosa yaliyokuwa yakifanywa na halmashauri yasijirudie katika benki.

## FIKRA MBADALA

# Nawatakia heri ya Krismasi na Mwaka Mpya



Pascal Mayalla

JAPO makala hizi ni za lugha yetu adhimu ya Kiswahili, naomba kutumia baadhi ya maneno ya Kiingereza kwa sababu baadhi yana ladha zaidi, ni matamu zaidi ya Kiswahili na yanakolea zaidi. Mfano mtu akikosea ni rahisi kusema 'sorry' kuliko kusema samahani. Ukimpenda msichana ukamwambia "I love you" ni neno tamu kuliko kumwambia "nakupenda".

Hata watu wakikasirika na kutukana kwa lugha ya Kiingereza, madhara yake ni madogo kuliko kutukana kwa Kiswahili. Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alikuwa anatumia sana maneno "nonsense" na "stupid" hakuna aliyekasirika lakini siku kiongozi mmoja mkubwa amewaita watu fulani "malofa na wapumbavu", kulizuka kelele. Hata sasa kuna kiongozi mmoja amewahi kumwita msaidizi wake 'nonsense' na 'stupid' hakukuwa na kelele.

Kwa vile kesho ni Krisimasi, sikukuu kubwa kabisa duniani kuliko nyingine yoyote, ambayo hutanguliwa na kitu kinachoitwa "festival mood" au "holiday mood", yaani mudi ya sikukuu au mudi ya kisherehe sherehe au ya kushereheka, naomba nami kujiunga na dunia nzima kuwatakia Heri ya Krisimasi na Mwaka Mpya, kwa kizungu, " Merry Christmas and a Prosperous New Year".

Tena sikukuu hii imedondokea siku nzuri ya Jumatatu na Jumanne, hivyo kwa wafanyakazi wa sekta ya umma na wale walioajiriwa rasmi na watu wa mshahara, wanajipatia kalikizo fulani ka mapumziko ya siku nne. Baada ya kwenda kazini Ijumaa, kazini tena ni Jumatano, raha iliyoje!

Lakini kwa sekta binafsi, kama sisi wenye uchumi wa kijungu jiko, tunaotegemea ajira ya vibarua au biashara ndogo ndogo, ili ule, lazima ufanye kazi au ufanye biashara, hivyo mapumziko ya siku nne ni majanga kwa baadhi yetu hasa sisi watu wa hali ya chini. Pamoja na hayo, naiona kama Krismasi hii haina shamrashamra. Lakini inawezekana kwangu tu na si kwa wengine!

Sasa kutokana na hii mudi ya kisherehesherehe na kwa vile sikukuu yenyewe imeletwa na Wazungu, Wamisionari walioleta dini ya Kikristo Afrika, kwenye kichwa cha habari cha makala hii kwa leo, nimeamua kuwatakia Heri ya Sikukuu ya Krismasi kwa kutumia lugha yake ya asili iliyokuja nayo, yaani Kiingereza, kwa kuwa inanoga zaidi nikitumia liugha hiyo.

Japo Krismasi ni sikukuu ya kuadhimisha kuzaliwa kwa Masiha, Bwana wetu Yesu Kristo, kwa sisi Wakristo, lakini inaadhimishwa dunia nzima na watu wa dini zote na mataifa yote. Hata nchi za Kiislam, kwa kitu kinachoitwa 'Chirstmas Spirit is Giving', yaani dhima ya Krismasi ni kutoa, kujitoa, kukipelekea zawadi kichanga kilichozaliwa leo.

Kwenye maisha yetu, si lazima kuwapo kichanga kilichozaliwa leo, hivyo hiyo dhima ya kutoa kwa waliotuzunguzunguka ukianzia kwenye familia yako, majirani waliokuzunguka, ndipo twende kwa ndugu, jamaa na marafiki hadi kwa wazazi wetu vijijini. N sikukuu ya kutoa na si ya kupokea.

Tena ukitoa, toa kwa moyo wote bila kujali ni dini gani, maana Krismasi ni sikukuu ya wote. Hata kwenye Dini ya Kiislamu, wanamtambua Masiya, Bwana wetu Yesu Kristo, ila kule wanamtambua kwa majina mengine. Kiislam wanamtambua Yesu kama Nabii Issa bin Maryam. Ukisoma sifa za huyo Nabii Issa bin Maryam, utakubaliana na mimi mtu huyo ni Yesu Kristo, ila kwa vile kila dini iko huru kuamini imani yake, kuna dini zinamkubali Yesu ndiye Nabii Issa, hivyo kuzaliwa kwake kunasherehekewa dunia nzima. Kwa maana hio Krismasi ni sikukuu ya wote.

Hata simulizi za mwanzo wa ulimwengu kwa dini kuu mbili za Wakristo na Waislamu, sote tunakubaliana dunia iliumbwa na Mungu, mwanzo Mungu aliwaumba Adam na Eva (Kikristu) au Adam na Hawa (Kiislamu), hivyo sisi binadamu wote ni watoto wa baba mmoja. Adam, hata neno mwanadamu, au binadamu, maana yake ni Mwana wa Adamu au Bin Adam. Hata sisi nembo yetu ya taifa ina mwanamke na mwanamume, Bibi na Bwana, wale ni wazazi wetu, Adam na Hawa.

Kwa dini zote mbili kuu duniani, Wakristo na Waislamu, tunaamini kisa cha Nabii Abraham (Kikristo) Ibrahimu (Kiislamu) na mkewe Sara (Kikristo), Sarai (Kiislamu), waliishi muda mrefu kwenye ndoa yao bila kubahatika kupata mtoto. Baada ya uzee kuwanyemelea na mkewe Sara siku zake kukoma, hivyo kutokuwa na uwezo tena wa kuzaa mtoto, ndipo akamtoa mjakazi wake wa Kimisri, Hagai (Kikristo), Hagir (Kiislamu), kushiriki na mumuwe Ibrahim, ili kupata mrithi.

Somo hapa ni familia ambazo hazikujaaliwa kupata watoto kutokana na tatizo la uzazi kwa mke, wanawake msiwe wachoyo kwa waume zenu, waruhusuni waume zenu kupata watoto kwa wanawake wengine. Hii ni endapo tatizo la uzazi ni kwa mwanamke, linapokuwa tatizo ni kwa mwanaume, hili mtanisamehe bado sijajua utaratibu wake, kwasababu hata kwenye vitabu vya dini, haijasemwa ila kwa maendeleo ya tiba za kisasa za kupandikiza ujauzito zinawezekana.

Huyo mjakazi akashika ujauzito, akamzaa mwana wa kwanza wa Ibrahimu akaitwa Ishamel (Kikirstu) Ismail (Kiislamu), aliyemzaa na huyo mjakazi wake wa Kimisri Hagai (Kikiristu), Hagir (Kiislamu). Familia nzima ilifurahi kupa mtoto, Baba, mama na mjakazi.

Baadaye kwa muujiza wa Mungu, mke wa Ibrahimu Sara, akiwa mzee wa umri wa miaka 80, alishika ujauzito, na kumzaa mtoto aliyeitwa Isaka (Kikristo), Isihaka (Kiislamu). Isumaili ndio Baba wa Waislamu wote, na Isaka ndio baba wa Wakisto wote.

Ni katika ukoo huu ndipo alikuja kuzaliwa Nabii Musa na aliyewakomboa Wairaeli kutoka utumwani Misri, na ndiye aliyepewa Amri Kuu za Mungu, ni zile zile amri alizopewa Musa kupitia Torati, na hata Yesu alipokuja, bado amri za Mungu ni zile zile. Yesu hakuja kuitengua Torati bali kuikamilisha, hivyo Wakristo na Waislamu ni watoto wa baba mmoja, tusherekee Krismasi pamoja.

Kuna Watanzania wengi wamejiandaa kwa mwaka mzima, ikiwamo kuweka akiba ya fedha za kutumia kula Krismasi, wanajikuta wanaisherehkea kinyume cha malengo. Badala ya kutoa, wao ndio kwanza wanatumia kwa kujipenda, kufanya matumizi makubwa na sherehe, kula, kunywa, kusafiri, kustarehe, kununua vitu na kujipa zawadi badala ya kuwapa zawadi wengine hasa wahitaji.

**I wish You A Merry Christmas and Prosperous New Year**

**Paskali 0784 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Ada za kuona wataalamu zisibague



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

GHAFLA nakutana na mshikaji wangu yuko haihai na ana shauku kubwa ya kuniambia kitu kilichomsibu asubuhi ya leo. Tunasalimiana na kumwuliza kulikoni, anafunguka kwa undani huku akisikitika.

Ananiambia anatoka kituo cha Polisi kuripoti yaliyomsibu, kwamba kuna jamaa kamshambulia na hivyo kuamua kumshitaki. Lakini anasema alipofika kituoni, askari aliyemkuta akamwomba kitu kidogo ili amfungulie jalada.

Maana yake ni kwamba kamwomba mlungula kinyume na wajibu wake wa kulinda raia na mali zake bila kuomba kitu. Lakini ananiambia hakuwa na kitu, hivyo akashindwa kutekeleza matakwa ya askari.

Akahoji iweje askari huyo kasomeshwa na serikali ili ahudumie raia lakini badala ya kufanya hivyo, anataka kuongeza matatizo kwa mwenye matatizo, kwamba kupigwa apigwe yeye na mfuko wake utobolewe. Nimemtazama na kumpa pole na kumshauri amwachie Mungu, kwa sababu aliyemfanyia matatizo hayo na aliyemwomba rushwa, wote 'mazi ga nyanza', iko siku nao watakumbwa na matatizo na kujutia. Wakati tumeachana, nikasikia suala lingine ambalo sasa hili ni la kitaifa lakini linanirudisha kwenye mkasa wa mshikaji wangu huyu. Hili ni suala la maboresho ya kitita yaliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Baada ya kutangaza maboresho hayo na kusema yamehusisha wadau mbalimbali na hivyo kuja na orodha na bei mpya za huduma na dawa, ghafla baadhi ya wadau wakaibuka na kusema hawajawahi kushirikishwa. Hasa ubishani mkubwa ukawa umejikita kwenye ada inayolipwa kuona madaktari wakutanapo na wateja wao, yaani wagonjwa, ambapo madaktari wabobevu wanatakiwa kulipwa mzigo mkubwa tofauti na wale wa chini. Lakini kulingana na maboresho hayo, inaonekana kiwango kimeshuka na hivyo kulalamikiwa na wadau hao, kwamba hailingani na kazi ya utaalamu wanayofanya.

Hili jambo hakika likanifikirisha sana kwamba kama madaktari wanastahili kupewa kiasi cha fedha ili kuhudumia wagonjwa kwa kuwasikiliza na kubaini matatizo yao na kuamua nini wafanyiwe kimatibabu, kwa nini jamaa yangu anamlamikia polisi!

Sikatai kuwa madaktari wanachukua muda mrefu kusoma na hata kupata ujuzi huo wa kulinda maisha ya kiafya ya binadamu. Lakini je, kada zingine nazo hazitumii muda mrefu kusoma na kutoa huduma kwa binadamu? Kwani polisi hatoi huduma kwa binadamu? Mbona hatakiwi kulipwa ili kuonwa na mteja ambaye ni mlalamikaji aliyetendewa visivyo. Kama daktari analipwa mshahara wake kila mwisho wa mwezi kwa nini fedha za kuonwa?

Tukiweka fikra zetu dawa, mimi nadhani mtu anayestahili kulipwa kwa kuonana na mteja ni mwalimu. Kwa nini? Kwa sababu bila mwalimu hakuna daktari, polisi, dereva, mhandisi na wataalamu wengine, lakini inashangaza ndio wanaolipwa kiwango kidogo sana.

Hebu angalia, awali ilikuwa ili kumwona daktari kwenye hospitali ya taifa, mgonjwa alitakiwa kukamuliwa Sh. 35,000 lakini sasa kupitia maboresho hivi sasa inatakiwa kuwa Sh 25,000, wataalamu hao hawataki masuala hayo.

Kumwona daktari bingwa mbobezi ilikuwa Sh. 25,000 na sasa ni Sh. 20,000 wakati katika hospitali ya mkoa, daktari mbobezi sasa atalipwa Sh. 25,000 kutoka Sh. 15,000 za awali. Daktari bingwa hospitali ya mkoa atalipwa Sh. 20,000 kutoka Sh. 15,000 huku katika kliniki bobezi kumwona daktari bingwa mboibnezi na daktari bingwa itabidi kulipa Sh. 10,000 kutoka Sh. 15, 000 za awali. Katika kliniki za kawaida, kumwona daktari bingwa na daktari mbobezi zitatutoka Sh. 10,000 tu za zamani. Huku kwenye afya ya msingi tuliko wengi, kumwona daktari ni buku au buku mbili tu. Alhamdulilahi! Lakini yote haya yanalenga kwa mwenye bima ya afya, lakini asiye nayo ndivyo hivyo, sharti ajiandae na hali hiyo. Siku zote mimi huomba kwamba kama kweli nchi hii ni tajiri kama tunavyoambiwa kwa nini utajiri huu usitumike kutulipia matibabu na ada za madaktari.

Maana yake, ni kwamba hapana sababu ya kuwa na bima bali bima iwe kwenye utajiri huo wa madini na maliasili kama ambavyo tumekuwa tukitamba kuwa sisi ni matajiri, hii ya kulipa baadhi ya wataalamu ada na wengine kuachwa wahudumie bila ada, inatia shaka.

Kama tunaona ni bora kuendelea na ada hizo, basi ifike mahali kila mtaalamu anayehudumia binadamu alipiwe ada hiyo, ili naye aishi maisha ya kitaalamu, kwa sababu tuna walimu bingwa na walimu wabobezi pia. Tunao polisi bingwa na polisi wabobezi pia.

Madaktari ni muhimu sana katika jamii kama walivyo watu wa kada zingine, kwa sababu kila mmoja ana mchango wake katika jamii, hivyo nao watazamwe kwa macho ya huruma kimaisha. Mungu tusaidie! Noel njema wasomaji wangu.

HABARI PICHANI

# PILIKAPILIKA ZA KRISMASI



Eneo la wafanyabiashara wadogo almaarufu 'Machinga' likionekana kuwa na mkusanyiko mkubwa wa watu wakitafuta mahitaji ya Sikukuu ya Krismasi Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wananchi wakiangalia maua ya mti wa Krismasi kwa ajili ya maandalizi ya Sikukuu ya Krismasi katika Mtaa wa Kongo Kariakoo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mteja akihesabu hela kwa ajili ya kulipia Mbuzi aliyemnunua katika Soko la Mbuzi Vingunguti kwa maandalizi ya Sikukuu ya Krismasi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mteja akichagua maua ya Krismasi katika eneo la wafanyabiashara Mwenge Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wananchi wakiwa katika pilikapilika za kununua bidhaa mbalimbali kwa ajili ya maandalizi ya Sikukuu ya Krismasi katika Mtaa wa Kongo Kariakoo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MAISHA

DESEMBA 24, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


**Chakula rahisi msimu wa sikukuu**

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Pamba nyumba vizuri msimu wa krismasi





Ukurasa 16




# MWANAMKE USAFI LAZIMA

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| N | ■ | U | H | U | R | U |
| Y | ■ | ■ | ■ | M | ■ | S |
| E | ■ | L | O | A | ■ | H |
| R | A | I | ■ | N | I | A |
| E | ■ | S | A | A | ■ | M |
| R | ■ | H | ■ | ■ | ■ | B |
| E | L | E | W | A | ■ | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

GUU, MBU, MBA, TEE, SHULE, ASALI, GAMBA, UBUTU, ELIMIKA, ENDESHA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI




## WATOTO

# PAKA RANGI



@MSAMBA

## CHEKA

MTOTO Peter alikuwa akimsaidia mama yake kumwagilia maji maua katika bustani iliyopo mbele ya nyumba yao.

Wakati wakiendelea kumwagilia maji Peter alimuuliza mama yake kuhusu tabia ya nyuki kupenda maua.

Peter: Eti mama kila kwenye maua kuna nyuki?

Mama: Ndio mwanangu, ni lazima nyuki watakuwa karibu na maua?

Juma: Kwani kila ua lina nyuki wake? Mbona mwalimu alituambia kila nyuki hufuata ua lake?

Mama: Hapana huo ni msemo unaomaanisha kila zuri linatokana na chanzo chake.

**SWALI**

**Taja matumizi tofauti ya chakula aina ya karanga**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kwa nini pendo la kwanza kwenye ndoa huchuja kasi?

MPENZI Msomaji, Wakati tunajiandaa kuufunga mwaka 2023 na kuukaribisha Mwaka Mpya wa 2024, liko jambo ambalo msomaji mwenzetu mmoja ameniuliza hapa kupitia ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani, nikaona ni muhimu tulijadili ili kuwekana sawa kwani hujitokeza kila kukicha ndani ya familia zetu.

Kwanza sikia ujumbe wake halafu niudadavue, kisha nawe msomaji utoe ya moyoni. Mambo hayo yapo, tunayashuhudia na kuyaona ni ya kawaida kumbe ni tatizo kubwa linalozitafuna familia zetu na ndio maana zinaishia kusambaratika.

Kumbe mambo yalianza kwa furaha, ibilisi akaingilia kati, mikataba ya ndoa mbele za viongozi wetu wa dini ikavunjwa na matokeo yake waliokula viapo vya nguvu, sasa wanapigana visogo, vikumbo. Kulikoni? Sikia ujumbe huu ulioletwa kama swali, halafu nawe utoe maoni yako.

"…..Anti napenda kujua ni kwa nini baadhi ya wanandoa wanakua na furaha na mapenzi ya dhati ile miaka ya mwanzo tu, baadaye hali inatoweka?

Nimeuliza kwa maana utakuta wanandoa wengine wanatumia gari moja ya familia kwenda kazini wanaweza kutoka nyumbani mpaka makazini mwao hutaona kicheko wala tabasamu, wamenuna hao utashangaa!

Utakuta wengine wakitoka nyumbani furaha tele wanatamani wasifike upesi. Utawaona kwenye foleni wakicheka, wakikumbatiana utajua tu hawa ni wapenzi wapya.

Wapo wale wenzangu na mimi utakuta ametoka nyumbani kanuna na akifika kazini vicheko vingiii… lakini akirudi nyumbani kanuna. Anti naomba tulijadili jambo hili. (Jonas Athanas, Mbeya)" .

Mpenzi msomaji, hapa mdau wetu huyu katika ujumbe wake amezungumzia maeneo mazito na ya msingi sana. Kwanza nianze na swali lake kwamba kwa nini wanandoa wanakua na furaha na mapenzi ya dhati ile miaka ya mwanzo tu.

Unajua pale mwanzoni bado yale mapenzi ya kabla ya uchumba, kisha ndoa yanakuwa bado moto moto. Kila kitu wanaelezana na ikiwezekana kila mahali kwenye mialiko au kutembelea ndugu wanaongozana au wanapeana ruksa.

Ngoja azaliwe mtoto wa kwanza. Shauku ya kupendana inaanza kupungua hasa kutokana na ukweli kwamba mama anaanza kuweka mkazo zaidi katika kumlea mwanae, huku baba naye akipata fursa ya kuchati na marafiki zake na pia kujikita zaidi katika kazi.

Kadiri watoto wanavyoongezeka ndivyo penzi linapungua na wivu unachipuka. Mama yuko bize na watoto, baba naye anapata mwanya wa kufanya mambo yake na ndipo pia anapopata fursa ya kutafuta mahusiano ya nje au kurejea mchuchu wa awali kabla ya ndoa kama alikuwa naye.

Wengine ndipo huanza kuchelewa kurejea nyumbani na kumfanya mama aanze kuuliza kulikoni. Kwa kinababa wengine huanza kuwa wakali wanapoulizwa na kuanza kutoa kauli za kukatisha tamaa.

Pointi nyingine aliyouliza msomaji wetu hapo juu ni kuhusu wale wanandoa wanaotoka nyumbani ndani ya gari moja hadi maofisini wakiwa wamenuna hakuna kicheko hata kimoja.

Mpenzi msomaji, hawa wako wengi tu wenye mtindo huo. Ukiona hivyo ujue nyumbani huko moto unawaka hakukaliki. Lazima wameamka na visirani vya jana yake pengine mume alichelewa kurudi, mke alitoka bila kutoa taarifa au kuna kutoelewana katika jambo fulani la kifamilia na kadhalika.

Na watu wa aina hii wengine wana makubwa zaidi yaliyojificha. Kwa mfano, kama wanalala kitanda kimoja na visirani vyao, basi watalala mzungu wa nne Si unajua (kama sikosei) ile karata 'K' ambayo wazungu wamegeuka kwa kichwa ni mguuni na mguuni ni kichwani. Upo hapo?

Ukiona hivyo, ujuwe tayari ndoa imeingia shubiri. Lipo jambo lkimesababusha. Kumbuka hakuna jambo linalotokea chini ya mbingu lisilokuwa na chanzo. Lazima ipo sababu kwa nini litokee.

Msomaji wangu, wengi unakuta hawajuani vema kule walikotokea (chimbuko). Hata tabia wengine hujificha lakini huziibua baadaye.

Anaweza kuwa alikuwa mlevi lakini hakuonyesha hivyo mwanzoni. Au alikuwa mpenda wanaume au wanawake lakini hakuonyesha hivyo. Sasa baada ya ndoa na kuanza kupata watoto, ndipo tabia nyingi huibuka.

Na tabia zingine siyo za asili bali za kuiga kwa wengine. Fulani anakunywa pombe, nami kwa nini nisinywe. Wengine husumbuliwa na mizimu ya kwao, roho za mitaa, au maagano ya ukoo.

**Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Kubariki mashoga ni kunajisi katiba, maandiko matakatifu

KUNA kila dalili miaka michache ijayo tukaanza ujenzi wa hosteli maalum za kuwalinda watoto wetu wa kiume wanaosoma ili kuwaepusha na janga la ushoga.

Kumekuwapo na minongiono kuhusu kauli ya Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, ambaye amenikuliwa na baadhi ya vyombo vya habari vya kimataifa kwambaameridhia mapadri kubariki ndoa za wapenzi wa jinsia moja.

Wakati hayo yakiwagawa wanaharakati, baadhi ya watetezi wa LGBTQ (mapenzi ya jinsi moja) wao wanashangilia. Ushoga si haki za binadamu bali ni ni dhambi kwa mujibu wa maandiko matakatifu.

Kwanza, ushoga ni jinai katika baadhi ya nchi, ikiwamo Tanzania, ambayo haikubaliani nao katika Sheria ya Makosa ya Kujamiana (SOSPA) ya Mwaka 1998 na Marekebisho yake ya Mwaka 2002.

Makosa yote ambayo ni kinyume cha maumbile, yametajwa katika Sheria Namba 47 ya Mwaka 1954, Kifungu cha 3 na namba 4 cha Mwaka 1998 Kifungu cha 16.

Sheria hiyo imeeleza kwamba mtu yeyote atakayekuwa ametenda kosa, atawajibika kwa kifungo cha maisha na wakati mwingine kifungo kisichopungua miaka 30.

Jambo hili ambalo ni dhambi na jinai, haliwezi kuwa haki za binadamu. Kwa hiyo, mashoga ni binadamu, kwa sababu hakuna mnyama shoga.

Iko hivi! kuwa kwao binadamu, kusiwafanye waone ni haki yao kuwa mashoga. Ushoga sio haki. Ushoga ni laana. 'Period'

Udhaifu wa viongozi wa dini, baadhi yao kukubali kubariki mashoga ni kunajisi katiba, maandiko matakatifu.

Hakuna mahali katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imeeleza kwamba ushoga ni haki. Wala hakuna mahali katika Biblia Takatifu na Qurani Tukufu imeandikwa ushoga ni haki.

Ni kweli tunataka kutungwa sheria, lakini wengi wetu hatuna uelewa tatizo ni kubwa kiasi gani kwenye jamii yetu, maana watu wanasema tatizo limeongezeka lakini ukiwauliza ni kwa kiasi gani hawajui.

Ni kubwa sana, ni kubwa sana kwa kiasi gani hatujui! Kwa hivyo ni muhimu tume yetu ya kurekebisha sheria, ifanye utafiti.

Ikishafanya utafiti, basi upande wa serikali iutazame huo utafiti, ingawa naamini kwamba utawapa taarifa muhimu kuona namna ambavyo mabadiliko yatafanyika.

Tume ya Kurekebisha Sheria, bado iko kimya kuhusu maboresho ya sheria hiyo ya kuzuia mapenzi ya jinsia moja.

Hatujaambiwa mpaka sasa, ni lini Muswada wa Sheria hiyo utapelekwa Bungeni kufanyiwa marekebisho yake.

Kama tunataka watoto wetu wakae salama, na vijana wetu wakae salama na taifa letu liwe salama, ni lazima Sheria hiyo ya SOSPA ifumuliwe haraka.

Kwa muktadha huo, nchi kama nchi, kwa sababu sheria hutungwa kulingana na mazingira yetu, na Sheria ya Makosa ya Kujamiana, lakini pia Sheria ya Makosa ya Jinai, inavyo vifungu mbalimbali vinavyohusu jambo hili.

Sasa ikiwa yako mapungu kwenye hivyo vifungu ambavyo viko kwenye sheria, Tume ya Kurekebisha Sheria, izibe mianya yote na wanaotiwa hatiani, Sheria ichukue mkondo wake.

- ***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com. Simu ya mkononi: +255 715 545 490***

# HARUSI











Ilikuwa siku ya furaha kwa Dk. Mauma Joseph na mkewe Sophia Ndosy baada ya kufunga ndoa katika kanisa la Waadventista Wasabato Nyegezi jijini Mwanza, Desemba 10, mwaka huu. Tunawatakia maisha mema ya ndoa.

# MITINDO

## MSULI VAZI LA HESHIMA



KATIKA maeneo ya ukanda wa pwani vazi la msuli linabeba maana ya kipekee ya ufahari na kuheshimika ndani ya jamii.

Msuli huwezi kufananisha na vazi lingine kwa umaalumu wake, kwani mtu anayevaa ni utambulisho tosha kwamba ni mtu mwenye heshima, busara na upendo wa hali ya juu.

Ndani ya ukanda wa Pwani vazi la msuli huvaliwa na watu wenye umri wa wastani na kuendelea na mara nyingi huvaliwa nyumbani, matembezi na hata kwenye shughuli muhimu za kijamii.

Kuna aina nyingi za misuli, lakini vazi pendwa ni lile lililonakshiwa mistari ya visanduku au mistari minyoofu kuzunguka upande wa nguo.

Katika tabia za Pwani, baba ndiye anaruhusiwa kuvaa msuli kwa sababu inaaminika ndiye kiongozi na mwenye mamlaka ndani ya nyumba.

Inapendeza zaidi msuli ukavaliwa na kofia ya kufuma kichwani na fulana iliyoambatana na koti juu yake.

Haipendezi kama miguuni utavaa viatu vya ngozi au raba, kiatu cha wazi au makubazi ndio inakupa mwonekano mzuri zaidi.

Wakati wa kuvaa ni lazima utambue aina ya ufungaji wa msuli, baadhi ya watu wanasema ufungaji wa pindo mbili mbele ndio halisi na unaopendeza.


Watu wengi wanadhani unapotaka kuvaa msuli hautakiwi kuwa na nguo nyingine ndani, dhana hiyo sio ya kweli kwani ni lazima kuvaa nguo ya kitambaa laini kiasi ndani ili kukupa uhuru wakati wa kutembea au kukaa.

Kwa ujumla vazi la msuli haliwezi kupotea kama yalivyo mengine, litaendelea kutumika miaka mingi ijayo kutokana na umuhimu wake katika jamii ya ukanda wa Pwani.



## UREMBO

**Na Mary Geofrey**



# MWANAMKE USAFI LAZIMA

UTATIA aibu kama utasuka 'wev-ing' lako wiki mbili hadi nne na usilisafishe maji kichwani.

Haijalishi uko wapi na unafanya nini, ila kukaa na nywele za bandia muda mrefu pasina kuosha na maji ni ishara ya uchafu kwani inaleta kero wakati huu wa msimu wa joto kali.

Nywele za bandia hutakiwi kukaa nazo muda mrefu, unatakiwa kufumua na kuosha kichwa wakati wote. Watu wanaweza wasikwambie ukweli ila ukawa kero wakati watu wanasherehekea sikukuu.

**USAFI WA KUCHA**

Hii tabia ya watu kufuga kucha pasipo kujua namna ya kuzitunza ni shida tupu. Kama unajijua huwezi kutunza kucha zako usifuge kufuata mkumbo kucha zinahitaji usafi.

Kumbuka mikono inashika vingi, inagusa sehemu zote za mwili kama hazitakuwa safi zinakusababishia madhara.



USAFI WA KWAPA

Umevaa nguo ya kukata mikono kwapa lina nywele, hapo maksi zinapungua, za nini? Hakikisha kwapa lako liko safi kabla hujavaa nguo ambayo haina mikono.

Jikoni unatakiwa usivae nguo ya wazi ili jasho la kwapa linalotokana na nywele nyingi lisiingie kwenye mapishi yako.

Ondoa nywele kwapani kwani itakupa uhuru hata unapokuwa umekaa na wageni waliokutembelea kipindi cha sikukuu.



## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Chakula rahisi msimu wa sikukuu

WAKATI huu wa msimu wa sikukuu watu wengi wanafikiria kupika chakula kizuri kama pilau nyama, kuku, mbuzi au firigisi.

Mara nyingi chakula hiki huliwa hasa wakati wa mchana na usiku wengi hushindwa kula kwa sababu ya kushiba sana mchana au kukosa mbadala wa chakula.

Leo tutaelekezana aina ya chakula cha ndizi nyama ambacho tutakula wakati wa usiku na ni rahisi sana kuandaa na kupika.

**Mahitaji**

Mahitaji ni nyama, ndizi bukoba, viazi kama utapendelea, nyanya, karoti, pilipili hoho, nazi, pilipili mbuzi vitunguu, chumvi na mafuta vyote utakadiria kulingana na kiwango cha chakula unachopika.

**Namna ya kupika**

Osha nyama kisha katakata kulingana na vipande vya ukubwa unaopendelea, changanya nyama, chumvi na tangawizi iliyopondwa.

Ongeza vikombe viwili vya maji kisha bandika kwenye sufuria maalum la kupikia kwenye jiko la umeme na uache kwa muda wa dakika 20.

Wakati nyama ikiiva, paka mikono yako mafuta kidogo ya kupikia kisha menya ndizi na viazi, vikate na uviweke kwenye sufuria yenye maji safi. Baadaye andaa mahitaji mengine kama kitunguu, karoti na pilipili hoho.

Ukipika nyama, subiri presha iishe kisha fungua mfuniko wa sufuria yako kisha changanya ndizi, viazi, viungo vyote na mafuta. Funika tena na pika kwa muda wa dakika 10.

Muda wa kupika ukiisha ondoa presha kisha weka tui na acha ichemke kwa muda wa dakika 5 jiko likiwa wazi. Chakula kitakuwa tayari na kipeleke mezani ukafurahie wewe na uwapendao.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Pamba nyumba vizuri msimu wa krismasi

NI msimu wa sikukuu, kipindi ambacho kinakuwa na pilikapilika za hapa na pale katika nyumba, kukiwa kunaonekana kutawala mapambo yanayoshabihiana na msimu wenyewe.

Katika ofisi na sehemu mbalimbali ukipita au kuingia, unakutana na mapambo ya sikukuu ikiwamo mti wa Krismasi ukiwa ndiyo umetawala.

Katika makala hii ya nyumba tunakupa dondoo kidogo kukuongezea baadhi ya vitu ambavyo vitachagiza msimu wako wa mwaka huu kuwa mzuri zaidi na ukaufurahia ukiwa nyumbani kwako.

Naamini kwamba katika kipindi hiki, familia nyingi huwa zinaungana katika mapumziko ya mwisho wa mwaka. Kwa hiyo ni muhimu kukifanya kipindi hiki kikawa ni cha furaha zaidi kwa mapambo tofauti ya sikuu ndani ya nyumba.

Mbali na mti wa Krismasi, pia yako mapambo mengine tofauti hilo, kama hutoweza kupata mti, unaweza pia kutafuta aina nyingine ya mapambo ambayo huenda yasikugharimu kabisa au ukayapata kwa gharama kidogo.

Lengo ni kuhakikisha nyumba yako inachangamka na kuipa raha familia ambayo imekusanyika nyumbani kwa ajili ya mapumziko ya mwisho wa mwaka.



Unaweza kuchanganya na mapambo mengine tofauti kama 'wall papers' na maua mengine kwa kuzingatia rangi zinazoshabihiana na msimu wenyewe.

Kwa mfano mapambo mengine ambayo yanaweza kutumika Krismasi ni pamoja na karatasi za rangi, taa za kung'aa, mapambo ya karatasi yanayotengenezwa kwa mtindo wa nyota.

Mengine ni kengele za Krismasi, picha za kondoo, farasi, mipira ya kung`aa, wanyama wadogo wa kutengenezwa kama kondoo.

Mapambo mengine ambayo unaweza kutengeneza ni ya maua ya asili kwa kuyaweka katika chombo au chupa maalumu ambacho kinaweza kuwekwa hata juu ya meza.

Pamoja na kupendezesha nyumba, pia hewa na harufu hubadilika na kuwa nzuri zaidi kutokana na maua yanayowekwa ndani.

Unaweza kupamba pia maneno yenye ujumbe maalum ambayo unaweza kuyaandika mwenyewe ya kuendana na msimu au ukayanunua katika sehemu maalumu yanapopatikana.

Hakikisha unaweka mapambo sehemu ambayo ni salama na hayawezi kuharibika kwa namna yoyote au kuharibiwa na watoto.

Pia nyumba katika musimu huu inatakiwa iwe inapigwa nyimbo zinazoshabihiana na msimu wenyewe.

Baada ya kuisha kwa musimu unatakiwa uyaondoe na kudizaini upya muonekano wa nyumba yako.

## DONDOO

### Vibuyu vinavyonogesha mandhari

Na Restuta James

WATAALAMU wa mapambo ya nyumba wanaeleza kuwa hakuna tena sababu ya mtu kutoyapendezesha makazi yake kwani vitu asilia vinaendelea kufanya vizuri.

Vibuyu ni moja ya vitu asilia vinavyotajwa kuboresha mazingira ya nyumbani na ambavyo vikitumiwa vizuri, vinatengeneza uasilia unaotuliza akili uwapo nyumbani.

Mtaalamu wa mapambo ya nyumba, Agnes Samson, anasema vibuyu vinafaa zaidi kutumika kwa kupanda maua ya kuning'inia yanayotumia maji kidogo.

"Kama unavyojua, kibuyu kikipata maji mengi kitaoza ndio maana tunashauri kipandwe maua yanayotumia maji kidogo ambayo unaweza kumwagilia mara moja kwa wiki," anasema.

Anasema vibuyu vinaweza kutumiwa bila kuwekewa nakshi au kwa kupolishiwa na kuchorwa michoro inayovutia kadiri mtu anavyopenda.

"Wengine wanapendelea kuchora ndege au kupaka rangi kwa namna ya kuvutia. Hata hivyo, tunashauri zaidi kupolishi ili kubakisha mwonekano wa uasilia," anasema Agnes.


Anashauri kwamba kwa wale wenye eneo kubwa la bustani, wanaweza kutengeneza vibuyu kwa namna ya kiota cha ndege na kukitundika kwenye mti bustanini ili kuwavutia kutua na kufanya makazi.

Mbali ya matumizi ya bustani, vibuyu vinafaa kutumika kama pambo kwa kufanywa 'holder' ya taa au kutundikwa karibu na taa kwenye korido, sehemu ya kulia chakula au kibarazani.

Kwa mwaka 2023, vibuyu na mapambo mengine ya asili ni vitu vilivyoshika kasi na hata bei zake ni kubwa sokoni na hasa katika nchi zilizoendelea.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
ULIWAAHIDI WAPIGA KURA SIKUKUU ZOTE UTAWACHINJIA WANYAMA
'NANI KALETA MNYAMA ANALALAMIKA SIJAMCHINJIA?' MTAJE
SHOBOKA KWENDA MKESHA WA KRISIMASI UONE!
KWA PICHA NINAYOIONA SHOBO ITOKE WAPI?'
'NDO NSHASEMA' KAMA ALISHINDWA KUKUHURUMIA BOSI WAKO KAZINI, BASI NA WEWE HUNA HAJA YA KUWA NA HURUMA NA MSHAHARA
KWELI MSHUA' MANENO KUNTU JIVUTE HUKU GIZANI TUKUPE MAUA YAKO
SHEMELA ONDOA SHAKA JAPOKUWA NNA GETO MOJA TUKILEWA CHAKALI TUTAJIBANZA TU.
HALITAKI KUOA LINATEGEMEA WAKE ZA WATU WAZIMIKE NA MIPOMBE YA KRISIMASI 'LIPATE ASUSA!'
MMOJA WETU KIFO KINA-MNUKIA
WEWE NDIO MIMI TUNAANZAJE 'KUCHEKECHANA' AKITOKEA MFADHILI WA BIA AU POMBE?
AH! WEWE SIO MIMI... ZIKIKUKOLEA UNAANZA KUMSHAURI MFADHILI 'AACHE POMBE!' ASOMESHE
JANAUME GANI KRIDMASI YOTE HII WENZAKO WANAWAZA KWENDA KUKESHA BAR WEWE UNAWAZA KUKESHA NDANI KUNA NINI?
SIO BURE UNA LAZI YA MTALAKA WAKO
MUDA MWINGINE UNAPASWA KUJIVISHA MABOMU 'UNALEWEA' ADA ZA SHULE AKILI IKAE SAWA
RESTI IN' PEACE MSHAHARA WA 'DISEMBA'
*KINYUNYIZO CHA LEO...
LEWA WATOTO WAYASIMULIE YAKO ULIVYOLETWA UKIWA CHAKALI...

## HABARI KIMATAIFA

# Rais Tshisekedi aongoza matokeo ya awali

**KINSHASA,** DRC

MATOKEO ya Uchaguzi Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) yameanza kutolewa ikionyesha Rais Felix Tshisekedi anaongoza.

Hata hivyo, wagombea wa upinzani wameyakataa matokeo hayo na kudai yana udanganyifu na kutaka uchaguzi huo kurudiwa tena.

Matokeo ya awali yaliyotolewa kuanzia juzi ni ya kura zilizopigwa na raia wa nchi hiyo wanaoishi mataifa ya Afrika Kusini, Ubelgiji, Ufaransa, Canada na Marekani.

Tume Huru ya Uchaguzi (CENI) ilisema matokeo ya kura zilizopigwa nchini DRC yataanza kutolewa kuanzia jana jioni.

Katika kikao cha waandishi kilichofanyika katika mji mkuu Kinshasa, Rais wa CENI, Denis Kadima kwa mara nyingine alipinga ukosoaji unaofanywa na wagombea wa upinzani na waangalizi huru wa uchaguzi kuwa zoezi la upigaji kura lilitawaliwa na vurugu na lilikosa uhalali. Wakizungumzia uchaguzi huo, kikundi cha waangalizi wa uchaguzi kutoka kituo cha Carter cha nchini Marekani,walisema kulikuwa na ukosefu wa imani katika mchakato huo na mianya katika uwazi, kwenye daftari la wapiga kura. Wagombea watano wa upinzani waliitaka tume hiyo kuitisha uchaguzi mwingine kwa sababu kuongezwa kwa muda na kuwa wa siku mbili ni kinyume cha katiba.

CENI imeweka kituo kikuu cha kupokea matokeo na kuyatangaza kiitwacho Basolo mjini Kinshasa ambacho matokeo kutoka kila kituo cha kupigia kura yanatangazwa pindi yanapoingia.

Uanzishwaji wa kituo hicho ni moja ya sharti kuu la upinzani na mashirika ya kiraia, lakini yalisema ukosefu wa uwazi katika kura zilizopigwa zimerahisisha kuwepo kwa udanganyifu.

Tume hiyo imeweka siku ya mwisho ya kutoa matokeo kamili ni Desemba 3, lakini haijulikani kama muda huo utaongezwa kutokana na kurefushwa kwa siku za upigaji kura.

Kituo cha Carter kimetoa wito kwa tume kuchapisha matokeo katika ngazi ya mitaa na kwenye vituo vya kupigia kura na kwenye tovuti ya tume ili kuhakikisha kuwa mchakato huo unaaminika.

Mgombea wa upinzani Moise Katumbi, ambaye timu yake ilikuwa ikifuatilia zoezi la kuhesabu kura, alisema kuwa matokeo hayo mpaka sasa yanamuonyesha yeye ni mshindi.

Kanisa Katoliki la DRC ambalo lina nguvu nchini humo limeweka zaidi ya waangalizi 25,000 ambao wanafanya kazi ya kujumlisha matokeo ya uchaguzi. Walifanya hivyo pia wakati wa uchaguzi wa 2018, na walipinga matokeo yaliyotolewa na CENI.

Uchaguzi huo utaamua kama Rais Tshisekedi ataongoza nchi hiyo kwa muhula wa pili wa miaka mitano baada ya kushika nafasi hiyo kutoka kwa mtangulizi wake Joseph Kabila.

**BBC**



Kundi la wanajeshi wa Ufaransa wakielekea uwanja wa ndege kuondoka nchini Niger. **PICHA: FP**

# Israel sasa yaigeuza Gaza kifusi

**GAZA**, PALESTINA

HALI imezidi kuwa mbaya Ukanda wa Gaza baada ya Israel kuendelea kurusha mabomu usiku kucha wa jana na kusababisha raia 18 kuuawa.

Katika shambulio moja kombora liliangukia katika kambi ya wakimbizi na kuwaua watu hao katika mji wa Nuseirat.

Kulingana na vyombo vya Habari Palestina, watu katika kambi nyingine ya Bureij waliamrishwa na jeshi la Israeli kuondoka kuelekea kusini wakati vikosi vya ardhini vikikabiliana na wanamgambo wa Hamas. Hata hivyo, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limepitisha azimio ambalo linalotoa wito wa kupelekwa misaada zaidi ndani ya Gaza.

Hatahivyo azimio hilo halikuzungumzia usitishwaji wa mapigano.

Kituo cha Habari cha Palestina (WAFA) kilisema watu 18 walifariki na wengine kujeruhiwa katika shambulio la kombora lililoilenga nyumba moja huko Nuseirat eneo lililoko katikati ya Gaza.

Kombora lingine pia lililenga kuharibu kiwanda cha kusafishia maji kilichopo eneo la Jabalia kaskazini mwa Gaza.

Wakazi wa Bureij, eneo lililo karibu na Nuseirat waliamrishwa 'kuondoka mara moja kwa ajili ya usalama wao na kutakiwa kuelekea kusini katika mji wa Deir al-Balah.

"Twende wapi?" Ziad, mhudumu wa afya na baba wa watoto sita aliliambia Shirika la Habari la Reuters kupitia simu.

Madaktari wasiokuwa na mipaka walisema katika ujumbe waliotuma kwenye mtandaoi wa X, kwamba urushaji wa makombora ya kiholela unaofanywa na Israeli dhidi ya Gaza yameligeuza eneo la kaskazini kugeuka kuwa kifusi.

Wameongeza kusema kuwa katika hospitali ya Al-Nasser ambayo ipo Khan Younis, maiti za watu na wengine walioje-ruhiwa wanaendelea kuwasili kila siku.

Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa lilisema takriban robo ya makazi yote ya Gaza yameharibiwa na watu 500, 000 wanakabiliwa na janga la njaa.

**BBC**

# Ufaransa yajiondoa rasmi nchini Niger

**PARIS,** UFARANSA

UFARANSA imekamilisha shughuli ya kuwaondoa wanajeshi wake nchini Niger baada ya kutakiwa kufanya hivyo na serikali ya kijeshi ya nchi hiyo.

Hatua hiyo ya kuondoa wanajeshi inakamilisha miaka kadhaa ya utoaji wa msaada wa kijeshi katika taifa hilo na kuibua wasiwasi kuhusu kuwepo kwa ombwe katika vita dhidi ya vikundi vya itikadi kali vilivyosambaa katika eneo la Sahel.

Mkuu wa Jeshi la Ufaransa, aliliambia shirika la habari la AP kupitia barua pepe kwamba ndege ya mwisho ya jeshi hilo iliyowabeba wanajeshi iliondoka Niger juzi ikiwa ni siku ya mwisho iliyowekwa na utawala wa kijeshi ambao ulikata uhusiano na nchi ya Ufaransa baada ya mapinduzi yaliyofanyika Julai mwaka huu.

Nchi ya Ufaransa tayari ilitangaza kufunga ubalozi wake nchini Niger kwa muda usiojulikana.

Wakati wa ziara yake nchini Jordan siku ya Alhamisi, Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, alisema nchi yake itaendelea kujihusisha katika eneo la Sahel ambalo limekuwa likikabiliwa na mashambulizi ya mara kwa mara kutoka kwa waasi hao.

Utawala wa kijeshi wa Niger, ulieleza kuwa kukamilika mwisho wa ushirikiano wa kijeshi na Ufaransa ni mwanzo wa enzi mpya kwa raia wa nchi hiyo.

**DW**

## MAKALA

# MABADILIKO YA KATIBA NA SHERIA BADO NI MUHIMU



Na Magabilo Masambu

**Kuelekea mwaka 2024 wa uchaguzi wa serikali za mitaa ni muhimu tukafanya jambo kama taifa. Mfano mdogo tu, Ibara ya 46(1) na (2) ya Katiba yetu inampatia Rais wa nchi kinga ya kutoshitakiwa. Maana yake hili pekee linampa uwezo wa kufanya lolote bila kujali wala kuhofu chochote, isipokuwa utashi wake utakavyomtuma katika kuamua mambo bila kulazimishwa na sheria za nchi.**

MWENYEZI Mungu amekabidhi mamlaka ya kuiongoza dunia hii mikononi mwa watu. Watu hawa ni binadamu wanaofanya mema na mabaya kwa sababu ya kasoro za kibinadamu. Sheria zinatungwa na watu kwa ajili ya kudhibiti uhalifu na uvunjaji wa sheria pamoja na mambo yanayoweza kusababisha kutendwa makosa.

Sheria zinafanya kazi kuu mbili. Moja ni kutaka kukinga makosa kufanyika kwa sababu mtenda makosa anaelewa wazi kwamba nikifanya hili ili atakabiliwa na mashtaka ndiyo maana Katiba si jambo la siri ili kila mmoja asome aone nini akifanya atakuwa ametenda makosa.

Kazi ya pili ya sheria ni kuhukumu. Baada ya kuwa umekwisha kutenda makosa, sheria inakuwa wazi tu bahati mbaya watu wengi huwatupia lawama mahakimu kwamba wanawahukumu mahakamani, lakini kwa kweli wanafanya kazi ya kusimamia tu kile tulichokubaliana wenyewe kwa maana ya katiba na sheria za nchi, maana sheria inasema ukitenda hivi adhabu yake ni hii.

Kwa muda sasa pamekuwapo na mjadala kuhusu ama mabadiliko ya katiba au Katiba Mpya. Naona wengine wanadai tume huru ya uchaguzi yaani mambo ni mengi muda mfupi.

Mimi pia ni miongoni mwa watu ambao nadhani mabadiliko ya katiba ni muhimu sana kwa manufaa yetu sote bila kujali tunatoka chama gani, dini au kabila gani.

Ninasema hivyo kwa sababu upungufu wa katiba unapotokea unatugusa sote.

Kuelekea mwaka 2024 wa uchaguzi wa serikali za mitaa ni muhimu tukafanya jambo kama taifa. Mfano mdogo tu, Ibara ya 46(1) na (2) ya Katiba yetu inampatia Rais wa nchi kinga ya kutoshitakiwa.

Maana yake hili pekee linampa uwezo wa kufanya lolote bila kujali wala kuhofu chochote, isipokuwa utashi wake utakavyomtuma katika kuamua mambo bila kulazimishwa na sheria za nchi. Tunapozungumza juu ya mamlaka ya Rais, tunamzungumzia yeyote atakayekuwa Rais, leo tunaye Rais mwema kesho itakuwaje!

Kuna wakati hatuamini kwamba mambo haya yanaweza kutupata kwa kuwa sisi ndio wenye mamlaka, lakini mambo yanabadilika.

Tanzania hatukuwahi kuamini kama iko siku tutampata Rais mwanamke kwa sababu ya mfumo dume tulio nao, lakini ya Mungu mengi leo tunaye mama yetu anatuongoza vyema kabisa na mwenyezi Mungu amwongezee umri zaidi.

Tunaweza kudharau vyama fulani kesho vikashika madaraka kama ambavyo imetokea kwa baadhi ya nchi hapa Afrika halafu katiba ikiwa imebaki hivi ilivyo kutakuwa na usalama kweli? Binadamu tunajua tunakotoka lakini kesho yetu anaijua Mungu. Tunaweza tusione umuhimu leo kwa sababu tuliye naye leo anatenda tunayopenda lakini kesho tunaweza kuishia kulalamika tena.

Bahati nzuri nzuri Rais Samia Suluhu Hassan tangu aingie madarakani, ameonekana kuhitaji mazungumzo hata kama hayatakuwa ya asilimia 100 kwa kadri tunavyohitaji lakini tayari mwanzo na mwanga unaonekana.

Kama kukusanya maoni ya wananchi tena kwa ajili ya kuandika Katiba nyingine yanaweza kufanyika mazungumzo ya pamoja kwa ajili ya kukubaliana vifungu gani vifanyiwe marekebisho ili kuweka nidhamu ya watumishi wa umma bila kujali nafasi zao.

Wako baadhi ya watu wanasema mbona kuna mabadiliko kati ya awamu ya tano na ya sita kwani katiba imebadilika? Ni sawa kwamba ni kweli mabadiliko yapo bila mabadiliko ya katiba na ni kweli vilevile kuwa mabadiliko hayo yametokana na utashi wa Rais wa sasa.

Je, vipi kuhusu kesho tuko tayari kukubaliana na mabadiliko mengine yatakayotokana na Rais mwingine ambayo pengine atakuwa tofauti na wa sasa? Sasa kuondoa hizo tofauti mabadiliko ya katiba yanapaswa kunyoosha rula.

Bahati mbaya tu kwa baadhi ya watu ni kwamba unapozungumzia mabadiliko ya katiba, wao humtazama Rais aliyeko madarakani.

Kama wataona anayoyafanya yanawafaidisha, watasema hakuna haja ya mabadiliko ya katiba. Ikiwa atafanya ambayo hayawafaidishi watapiga kelele kwamba mabadiliko ya katiba ni muhimu. Tuliona wakati fulani kila mtu anapiga kelele sasa muda mfupi tu tumeshasahau.

Matumani na imani yangu ni kwamba kwa jinsi ninavyoona mwelekeo na nia njema ya Rais Samia tunaweza kupata katiba bora si katiba mpya. Jambo la msingi ni kushirikiana naye kwa nia njema, huku tukitambua kwamba nchi hii ni yetu sote tunahitaji kuijenga kwa pamoja.

Tuweke pembeni maslahi binafsi na ya vyama vyetu kwa sababu hatujui kesho tutaongozwa na nani. Vinginevyo ipo siku tutalia wote na tutakosa wa kutufuta machozi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Wanandoa wanapogeuka burudani kwa majirani, kisa ni kugombana*



Na Adam Fungamwango

**"Ninapata tabu moyoni mwangu mimi kwa kweli, nimekupenda wewe lakini hanijali mama. Tumekuwa sisi wawili kama sinema, hapa nyumbani kwetu kila siku kelele. Lakini kwa vile, tunaishi hapa kwa wazazi wako, mwenye sauti ni wewe.**

MUME anaporudi kazini tu, majirani wanakuwa wamepata burudani nyingine. Wanazima redio zao ili kusikiliza burudani ambayo kwao ni kama tamthilia kwenye televisheni.

Ni zogo tu moja kwa moja na mkewe. Haijulikana kama huwa wanamuangalia nje kama anarudi, au wanaanza kusikia vurumai ndani ndipo majirani wanapojua burudani yao imeanza.

Vyovyote iwavyo, majirani wameshawazoea watu hawa. Kuzozana na kuzodoana ni kitu cha kawaida.

Cha kusikitisha ni kwamba jambo hili linamuuma sana mume. Analia moyoni na kusikitika. Hana uwezo tu, lakini yanayoendelea hayampendezi.

"Ninapata tabu moyoni mwangu mimi kwa kweli, nimekupenda wewe lakini hanijali mama. Tumekuwa sisi wawili kama sinema, hapa nyumbani kwetu kila siku kelele.

Lakini kwa vile, tunaishi hapa kwa wazazi wako, mwenye sauti ni wewe. Naogopa fedheha mama oo mie, naona aibu kweli mpenzi, hapa ni kwa wakwe zangu sisemi lolote, fanya upendavyo."

Hapa tunaona kuwa kumbe, mke ndiyo mwenye matatizo. Mke yupo kwao. Jamaa anaishi ukweni kwa hiyo anakubali kila kitu anachofanyiwa kwa sababu anaogopa fedheha.

Nadhani pia jamaa anaogopa kama akiamua kuchukua hatua basi baba, mama mkwe na familia itakuwa upande wa binti yao, hivyo ikala kwake.

Haya ni mashairi yaliyomo kwenye wimbo wa 'Majirani Huzima Redio' uliorekodiwa kwenye studio za Redio Tanzania mwaka 1986. Haya mambo yapo kwenye jamii kwa sababu wanamuziki wa zamani hawakuwa wanatunga nyimbo kutoka hewani.

Walitunga kutokana na matukio yanayotokea kwenye jamii, yanayowahusu wao wenyewe, rafiki zao, watu wao wa karibu au majirani.

Huyu mume wanatatizwa maneno ya mkewe kwani amekuwa na gubu na kelele nyingi kiasi kila anaporudi kazini majirani wanaona ni fursa ya kusikiliza nini ambacho leo watagombania.

Mume anarejea nyumbani badala ya kupokewa kwa bashasha na mabusu na mkewe, anapokelewa kwa kejeli, maneno na dharau. Nadhani hapa jamaa badala ya kulalamika kama kweli hapendi dharau itabidi ajiongeze.

Aache kupenda bure, atoke akapange hata chumba kimoja ili arudishe heshima, aache kufokewa kila siku.

"Hata mwezi bado ooo hoo, tangu tuoane hee, kelele kila siku ndani ya nyumba yetu mama. Hata mwezi bado ooo hoo, tangu tuoane hee, kelele kila siku ndani ya nyumba yetu mama."

Hiki ni kiitikio cha wimbo huo, ambao unaonyesha kuwa kumbe ndoa yenyewe bado changa kabisa. Ndoa nyingi zina matatizo, lakini hii kiboko. Ndoa zina changamoto nyingi lakini huonekana miaka kadhaa baada ya kuoana.

Kwa kipindi cha mwezi mmoja huwa ipo kwenye hatua ya kwanza, ile ya kubembelezana, kudekezana na kuliwazana, hata kama ni kwa uongo uongo.

Hapa hakuna yoyote anayekubali kuiweka tabia yake halisi hadharani. Ni kipindi ambacho kila mmoja ni kama paka aliyeficha makucha yake hadi pale atakapohitaji kuyatumia.

Lakini utafika muda wa kuyatoa. Pale kila mtu atagundua tabia halisi ya mwenzake.

Kinachoendelea hapo sasa ni yale mazoea. Kwa sababu wameshazoea kukaa pamoja, basi kunakuwa na uvumilivu fulani kama tabia zenyewe za mmoja wapo au wote ni mbaya.

Siku zote tabia mbaya huwa zinachokwa. Baada ya uvumilivu wa muda mrefu hatimaye ndoa inaweza kuvunjika.

Ndoa haina tabia ya kuvunjika kwa siku moja, ila huanza kusambaratika taratibu na pale watu wanapoachana inakuwa ni kilele tu cha kuachana.

Watu huanza kuchana pale mmoja wapo au wote wanaposema. "He, sikujua, kumbe huyu ndivyo alivyo!"

Cha ajabu kwenye wimbo huu, mume anasema ndoa yake haina hata mwezi, lakini mke amekuwa kama spika, mtaa mzima wanamsikia akibwabwaja.

"Ninaporudi kazini majirani huzima redio ili watusikilize tunavyogombana, wametupachika majina wewe Pwagu na mimi Pwaguzi, kwa vile imekuwa ni mazoea, ingawa nimekuoa na pesa na pendo langu ee, tabia zako zimenishinda, aaaa nasikitika."

Mume anasikitika kuwa hata majina tena siyo mume na mke, bali ni Pwagu na Pwaguzi. Hapa sitaki hata kujua nani Pwagu nani Pwaguzi, wote ni wale wale tu.

Yaboa zimemshinda mume, lakini anasikitika. Nimesema hapa juu kuwa ndoa ndipo inapoanza kuvunjikia hapo.

Mume analalamika tena kwenye mashairi ya wimbo huo, kuwa katika nyumba yao hajulikani mume wala mke, wote kama kambale tu, baba, mama, mtoto wote wana ndevu.

Kwenye dunia hii, hata kundi la wanyama, huchagua kiongozi wao. Ndani ya nyumba kukiwa hakuna kiongozi thabiti hata familia inayumba.

**Tuma Meseji 0716 350534**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu-3

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

WAKATI geti linafunguliwa kuruhusu wagojwa, tayari Kassim alikuwa wa kwanza ndani ya wodi ya wanawake.

Akapata shida kidogo kwa sababu hawajui ndugu wa mgonjwa na hata mgonjwa mwenyewe hajamzoea kivile, kwa sababu mara zote humwona akiwa amekaa barazani.

Alizunguka karibuni akamalize wodi nzima. Ghafla akajikuta anaitwa.

"We baba Matokeo!" Akasikia anaitwa. Nusu acheke, lakini akajikaza na kuishia kutabasamu. Alikuwa mmoja wa rafiki za mgonjwa aliyepachikwa jina la mama Matokeo na yeye mwenyewe.

Akarudi nyuma kwenye kitanda cha mgonjwa. Akawaona rafiki zake wote wawili. Akakaa kwenye kitanda cha mgonjwa na kumuuliza maswali kadhaa na kumfariji. Mgonjwa alionekana kushangaa na kufurahi kwa wakati mmoja.

Moja ya mambo ambayo aliyotakuta hospitali ni bili ya pesa za matibabu. Ilikuwa shilingi elfu hamsini, iliyolipwa kwa mchango wa ndugu na jamaa ni shilingi elfu ishirini na tano. Aliomba cheti na kupelekwa eneo la kulipia. Akaenda kulipa nusu ya pesa iliyobaki. Ndipo kwa mara ya kwanza alipolifahamu jina la msichana yule alipolisoma kwenye cheti cha mgonjwa. Anaitwa Sauda Rajab.

*****************************

Hivyo ndivyo walivyofahamiana Kassim na Sauda. Ukaribu huo ndio baadaye uliwafanya wawe wapenzi.

Baba Matokeo na mama Matokeo, ukichanganya na kulipa nusu nzima ya bili ya matibabu iliwasogeza karibu zaidi. Uhusiano unaanza, na baadhi ya ndugu wakawa wanajua.

Sauda aligundua kuwa Kassim ni mlevi kupindukia, na kwa vile walishaanza uhusiano, kama kawaida ya watu wa uswazi wakampelekea faili lake kuwa alishawahi kuwa na mwanamke anayeitwa Siwatu ambaye alimchumbia lakini kabla hawajafunga ndoa yakatokea ya kutokea, jamaa akatendwa na ikamwathiri sana kichwani kiasi cha kutopenda kuwa na mpenzi yeyote.

Rafiki yake mkubwa ni pombe na imekuwa ikimuathiri sana kwani wanavyomuona anadhohofika na hayupo kama zamani.

"Kazi kwako Sauda, mwanamume ndiye huyo, wa kwako huyo, Mungu akupe nini tena shoga yangu, akupe donda upate kuchunga nzi? Tunamjua sisi alikuwa hataki tena mwanamke yeyote, lakini Mungu si Athumani kaangukia kwako. Haya tena hatutaki kusikia kingine tena. Mbuzi kafia kwa muuza supu." Mama mmoja anayemfahamu vyema Kassim alimuuma sikio Sauda.

"Sawa mama nitafuata ushauri wako." Sauda akaitika.

Ikawa kama alivyombiwa. Kuna siku Sauda alikalisha Kassim kikao kizito.

"Unasikia Kassim mpenzi, najua unanipenda na mimi nakupenda, penzi letu bado ni changa sana. Bwana wewe nasikia unakunywa pombe. Lakini nasikia huko nyuma ulikuwa hunywi, ila kuna mambo fulani fulani yamepitika huko, mimi mwanamke nimefundwa, siwezi kuyasema hapa, labda mwenyewe uamue kuniambia.

Mimi kama mpenzi wako nakuomba kuanzia leo achana na pombe. Siyo kama nakukataza moja kwa moja, kama kunywa unaweza kufanya hivyo moja, mbili tatu kwa ajili ya afya, siyo kwa ajili ya stresi. Kwa sasa mimi nipo, kuna na amani, nakuomba mpenzi wangu acha pombe."

Ulikuwa ujumbe wa Saida kwenda kwa Kassim.

Bila hata kutafakari sana Kassim aliona kuna ukweli. Alikuwa anakunywa pombe kutokana na stresi, lakini tangu ampate Sauda moyo wake ulitulia kama maji mtungini.

"Ni kweli na hata hivyo nimepunguza sana kwa sababu nataka muda mwingi tukae sote." Akajibu Kassim.

"Halafu kila siku kula kwa mama lishe au hotelini naona unapoteza pesa nyingi bure, halafu hata ubora wa chakula la ladha si kama cha kupikwa nyimbani. Kama hutojali, uwe unaniachia pesa kidogo tu niwe nakupikia chakula cha jioni. Angalau chakula cha jioni." Likikuwa ni ombi lingine la Sauda.

Kilichopo ni kwamba Sauda ambaye alitoka kwao Kondoa alikuwa anaishi pale na dada yake. Dada yake anafanya kazi ya kuajiriwa mjini. Naye baada ya kumaliza kidato cha nne aliamua kuja kumtembelea dada yake na kumsaidia kazi za hapa na pale nyumbani anapokuwa kazini.

Alichokuwa akiomba Sauda ni kwamba Kassim aongeze pesa, ili akichanganya na zile anazoachiwa na dada yake apike chakula kingi kwa ajili ya mpenzi wake jioni kwani anaona kama anahangaika sana kula cha mgahawani.

Kichwa kikamuuma Kassim. Kuna habari anasimuliwa na watu mbalimbali, kuwa baadhi ya wanawake wana tabia ya kutengeneza dawa ya mapenzi kwa wanaume ili wawapende zaidi au wawafanye wajinga.

Dawa hii wenyewe wanaiita libwata. Kassim, pamoja na kwamba anampenda Sauda, alichokuwa anaogopa ni visa anavyosimuliwa kuwa kuna baadhi ya wanaume wanakuwa mazezeta kabisa. Kumpenda si tatizo, lakini kufanywa kama msukule, kukubali kila anachoambiwa au kuwa zezeta na kushindwa kwenda hata kazini, ndiko kulikomtisha zaidi.

Pia aliambiwa dawa hii anatengenezewa mwanamume kwa kuwekewa kwenye chakula, hivyo alihisi kama Sauda anaweza kuchukulia nafasi hiyo kufanya hivyo. Akasita kidogo na kumwambia atafanya hivyo siku nyingine.

Mtoto wa watu Sauda akajiongeza. Si huwa anakwenda usiku wakati Kassim anakuwa amerejea kazini. Akaona hii ya kumwambia atoe pesa halafu anajivutavuta hapana. Kwa kutumia pesa zile zile za dada yake, alipika chakula cha jioni. Wali aliouunga kwa nazi na njegele. Alipakua mwingine na kuuweka kwenye hotipoti.

Saa mbili usiku aligonga hodi kwa Kassim. Alipofungua aliona mgeni wake kwa mara ya kwanza amekuja na kikapu kidogo. Akampokea na kukaa kama kawaida wanapiga stori. Lakini alisikia kuna harufu nzuri ya chakula kilichoonekana kitamu.

"Umekuja na nini leo mpenzi?"

"Chakula. Nimekuja nacho tule wote." Kassim aliona aibu kidogo, kwani alikumbuka aliambiwa atoe pesa kidogo lakini akapotezea.

Leo bila kutoa pesa analetewa chakula.

Sauda alitoa hotipoti kwenye kikapu chake, akaweka mezani. Alichofanya Kassim na kwenda kununua soda ili wakila washushie.

Kitendo cha Sauda kutaka kula na aliyemletea kikaondoa dhana ya Kassim ya kuwekewa limbwata.

"Ingekuwa hivyo yeye asingekula." akajiambia. Wakala kwa pamoja. Utamu wa chakula ulimshangaza Kassim.

"Umepika wewe hiki chakula?"

"Nani mwingine?"

"He, kama ni hivyo wewe kumbe ni mkali mpaka kwenye jiko!

"Nashukuru Mungu kwa hilo mpenzi."

Tangu siku hiyo, Kassim akawa anatoa pesa ya kula kwa Sauda ili awe anamletea chakula usiku.

Na si hivyo tu, hata kama siku dada yake Sauda akikwama, Kassim anachukua nafasi ya kurekebisha mambo watu wale. Ndipo alipoamini kuwa Sauda ni mwanamke ambaye pia anajua mapishi hasa. Hakurudia tena kula mgahawani.




**Kichwa kikamuuma Kassim. Kuna habari anasimuliwa na watu mbalimbali, kuwa baadhi ya wanawake wana tabia ya kutengeneza dawa ya mapenzi kwa wanaume ili wawapende zaidi au wawafanye wajinga.**

**INAENDELEA JUMAPILI**



# TEKNO HAJUTII TABIA YA KUJIPENDA

MWANAMUZIKI maarufu wa Nigeria, Augustine Kelechi, maarufu kama Tekno, amesema amekuwa na tabia ya ubinafsi kwa sababu ni mtu wa kujipenda kupita kiasi.

Amesema katika mahojiano ya hivi karibuni kwamba licha ya watu kuwa na mawazo mengi juu yake, anafurahia kuwa na hali hiyo.

Tekno ambaye ni mwenyeji wa Jimbo la Ebonyi amewashauri vijana kufurahia kwa kila jambo wanalolifanya kwa sababu hayo ni maisha yao.

# Hali ngumu kwa P Diddy


HALI inazidi kuwa mbaya kwa rapa mkongwe, P Diddy baada ya kampuni 18 kusitisha ushirikiano wao na jukwaa la kibiashara la Combs Empower Global.

Kulingana na ripoti ya Rolling Stone, kampuni hizo zimejiondoa katika jukwaa hilo kutokana na kesi za unyanyasaji wa kingono zinazomkabili msanii huyo.

Empower Global, iliyoanzishwa na Diddy mnamo 2021, ililenga kukuza biashara zinazomilikiwa na watu weusi kupitia soko la kidijitali.

Miongoni mwa kampuni zinazokatisha uhusiano wao na Empower Global ni kampuni ya mitindo ya House of Takura, ambayo ilithibitisha kujiondoa.

"Tunachukulia tuhuma dhidi ya Combs kwa uzito mkubwa na tunaona tabia kama hiyo kuwa ya kuchukiza na isiyovumilika." Amesema mwanzilishi wake Anette Njau.



## ZISIKUPITE

### EN_NESYRI ANUKIA UNITED

KLABU YA Manchester United inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Sevilla na Morocco, Youssef En-Nesyri, mwenye umri wa miaka 26, kwa sababu mchezaji mwingine wa kimataifa wa Guinea na Stuttgart ,Serhou Guirassy (27), analengwa na Tottenham Hotspur. (***Sun***)

### HOJBJERG KUTUA SPURS

TOTTENHAM Hotspur inaweza kumkabidhi kiungo wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, mwenye umri wa miaka 28 kwa Chelsea kama sehemu ya makubaliano ya kumsajili mchezaji wao wa kimataifa wa England, Conor Gallagher (23). (***Sky Sports***)

### WERNER ANUKIA VILLA

KLABU ya Aston Villa inamtaka kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner, mwenye umri wa miaka 27 kwa mkopo kutoka RB Leipzig huku wakitafuta kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. (***Football Insider***)

### DIOMANDE ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA imewasiliana na Sporting Lisbon ya Ureno kuhusu uwezekano wa kuwasajili beki wao wa Ivory Coast, Ousmane Diomande, mwenye umri wa miaka 20 na mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres (25) katika dirisha la Januari. (***Evening Standard)***

### ZUBIMENDI ATAJWA ARSENAL

ARSENAL inamtaka kiungo wa Real Sociedad, Martin Zubimendi, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, mwenye umri wa miaka 24 anasita kubadili klabu ifikapo Januari. ***(Football. London)***

### O'RILEY ATAJWA MILAN

INTER Milan inaandaa ofa kwa kiungo wa Celtic, Matt O'Riley kwa usajili wa mkopo ifikapo Januari na kulazimika kumnunua mwishoni mwa msimu - lakini Aston Villa na West Ham pia wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye ni raia wa Denmark. (***Sky Sports***)

### EKWAH AGOMBEWA EPL

KIUNGO wa kati wa Sunderland, Pierre Ekwah, mwenye umri wa miaka 21 anawaniwa na klabu za Crystal Palace, Fulham na Nottingham Forest zote za England. (***Evening Standard***)

### LOKONGA KUREJEA ARSENAL

LUTON Town inafikiria kukatiza mkopo wa msimu mzima wa kiungo wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Albert Sambi Lokonga, mwenye umri wa miaka 24 ili kuimarisha nafasi nyingine. (***Teamtalk***)

### EVERTON YAINGIA SOKONI

KLABU ya Everton inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Burnley, raia wa England, Josh Brownhill, mwenye umri wa miaka 28 katika dirisha dogo la usajili la Januari. (F***ootball Transfers)***

### ANDRE, FULHAM KIMEELEWEKA

FULHAM imekubali mkataba na Fluminense kwa kiungo Andre na sasa ni juu ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 22 kuamua kama anataka kuhamia Craven Cottage. (***Football Insider***)

### TRAORE KUSAJILIWA SEVILLA

KLABU ya Sevilla inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Hamed Traore, mwenye umri wa miaka 23. (***AS***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: NIMEFUNGA UKURASA WA CITY 2023

## Ni baada ya timu hiyo kutwaa taji la Klabu Bingwa ya Dunia juzi na...

**JEDDAH,** Saudi Arabia

PEP Guardiola amesema "nimefunga kurasa" baada ya Manchester City kutwaa taji la Klabu Bingwa ya Dunia hapo juzi.

City walitwaa taji lao la tano kwa mwaka huu baada ya kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Fluminense katika mechi ya fainali iliyochezwa mjini, Jeddah na kumfanya Guardiola kushinda kila taji tangu atue hapo kama kocha wa klabu hiyo mwaka 2016.

Guardiola alisema kazi yake "imekamilika" lakini ikiwa imesalia miezi 18 kwenye mkataba wake, alisisitiza bado ana ari ya kushinda mataji mengi zaidi.

"Ni siku nzuri na nzuri sana," alisema Guardiola.

"Nimefurahishwa sana na ningependa kusema tulikuwa na hisia tutafunga ukurasa, tulishinda mataji yote, hakuna kitu kingine cha kushinda. Nilikuwa na hisia kazi imekamilika.

> **"Sasa ni wakati wa Kris masi, tunanunua kitabu kingine na kuanza kuki andika tena. Miaka nane iliyopita, imekwisha."**

Kombe la Klabu Bingwa la Dunia ni taji la 14 kuu kwa Guardiola kama Kocha wa Manchester City baada ya mataji matano ya Ligi Kuu, mawili ya Kombe la FA, manne ya Kombe la Carabao, moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Super Cup.

Guardiola mwenye umri wa miaka 52, yuko chini ya mkataba pale Etihad hadi mwaka 2025 baada ya kusaini mkataba mpya wa miaka miwili hapo Novemba, mwaka jana.

"Ninafunga sura, ni kwa miaka nane ya kazi ya ajabu nyuma ya pazia," aliongeza.

"Nilikuwa na hisia mataji yote unaweza kushinda, tumefanya. Haiaminiki tulichofanya. Tunajaribu kununua kitabu kipya na kuanza kuandika historia nzuri.

"Wachezaji waliokonje bado wana njaa na motisha, nimefurahishwa na watu wengi katika klabu kwa miaka mingi. Sikufikiria tulipofika Manchester tunaweza kufanya hivi na kumaliza na taji la Klabu Bingwa ya Dunia."




# SUÁREZ AUNGANA RASMI NA MESSI

**MIAMI,** Marekani

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Luis Suárez, amekamilisha uhamisho wa kuijiunga na Inter Miami, na kuhitimisha kuungana tena na mchezaji mwenzake wa zamani wa Barcelona, Lionel Messi, klabu hiyo ya Ligi Kuu Soka ya Marekani maarufu MLS, imethibitisha.

Suárez (36), anahamia Miami kama mchezaji huru baada ya kuondoka Grêmio ya Brazil, ambako alicheza mechi 53 katika mashindano yote msimu uliopita na kufunga mabao 26.

Mabao yake 17 ya ligi yaliisaidia Grêmio kumaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Serie A ya Brazil na kumwona akishinda Mpira wa Dhahabu kama mchezaji bora zaidi katika kitengo hicho.

Suárez alisaini mkataba wa mwaka mmoja na Inter Miami ambao utamfikisha hadi mwisho wa msimu wa 2024.

"Tuliahidi mashabiki wetu tutawafuata wachezaji bora zaidi duniani ili kujenga kikosi ambacho kinaweza kushindana katika viwango vya juu kabisa vya Bara la Amerika," Mmiliki Mkuu, Jorge Mas, alisema katika taarifa iliyowekwa na klabu hiyo.

"Tukitoka katika msimu wa kushinda tuzo nchini Brazil, Luis atakuwa nyongeza muhimu kwa orodha yetu. Tutaendelea kuwa na tamaa na daima kujitahidi kutafuta uhuru wa ndoto."

Uhamisho wa kwenda Miami, ambao unamfanya Suárez kukatiza mkataba wa miaka miwili aliosaini na Grêmio, unamkutanisha na wachezaji wenzake wa zamani wa Barcelona ambao ni Messi, Jordi Alba na Sergio Busquets. Wachezaji hao wanne walitumia misimu sita pamoja Camp Nou kati ya mwaka 2014 na 2020, wakishinda mataji manne ya LaLiga na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nina furaha sana na nina furaha kuchukua changamoto hii mpya na Inter Miami," Suárez alisema katika taarifa hiyo. "Siwezi kungoja kuanza, na niko tayari kufanya kazi ili kufanya ndoto ya kushinda mataji zaidi na klabu hii kubwa kuwa ukweli. Nina matumaini juu ya kile tunaweza kufikia pamoja na matarajio yetu ya pamoja.

"Nitajitolea kuwaletea furaha mashabiki hawa wazuri ambao nimesikia mengi juu yao wakati nikivaa rangi za Inter Miami, na ninatarajia kuungana na marafiki wakubwa na wachezaji. Pia nina hamu ya kukutana na wachezaji wenzangu wapya na makocha."

## Varane atajwa kurejea Madrid

**MADRID,** Hispania


KLABU ya Real Madrid huenda ikajaribu kumsajili tena beki wake wa zamani ambaye kwa sasa anaichezea Manchester United, Raphael Varane, baada ya beki wao kutoka Austria, David Alaba (31) kupata majeraha ambayo yanatarajiwa kumweka nje kwa muda mrefu.

Hata hivyo, inaonekana kutakuwa na ugumu kumpata Varane katika dirisha hili la Januari kwa sababu Kocha wa Mashetani Wekundu, Eric ten Hag, hayuko tayari kumwachia kwa sasa.

Varane mwenye umri wa miaka 30 alijiunga na Manchester United mwaka 2021, msimu huu amecheza mechi 14 za michuano yote na mkataba wake wa sasa unamalizika msimu ujao.

Awali, beki huyo kutoka Ufaransa alikuwa anahusishwa kuwindwa na baadhi ya vigogo kutoka Saudi Arabia ambao walimhitaji tangu dirisha lililopita.

Ilidaiwa Erik ten Hag hakuwa na uhusiano mzuri na staa huyu hadi akawa anamweka benchi kwenye mechi kadhaa zilizopita lakini kwa sasa wanadaiwa kuyamaliza na kila kitu kipo sawa.




# Mwekezaji wa United kucheleweshwa

**MANCHESTER,** England

UWEKEZAJI wa Sir Jim Ratcliffe wa pauni bilioni 1.5 katika Klabu ya Manchester United hauwezi kukamilishwa hadi baada ya dirisha la uhamisho la Januari, vyanzo vimeiambia ESPN.

Imeelezwa mchakato huo hautakamilika mapema hata kama dili la kununua hisa la asilimia 25 ya klabu hiyo litathibitishwa kwenye soko la fedha katika siku chache zijazo.

Ratcliffe na Kampuni yake ya INEOS amekuwa katika majadiliano ya kina na wamiliki wa United, familia ya Glazer tangu Oktoba, mwaka huu na kuhusu mpango huo ambao utampa bilionea huyo wa udhibiti kamili wa uendeshaji wa soka katika klabu hiyo.

Vyanzo viliiambia ESPN mazungumzo yako katika hatua za mwisho na ucheleweshaji wa hivi karibuni unatokana na sababu ya maelezo ya kisheria ya pande zote mbili kukaguliwa kabla ya mikataba kusainiwa.

Tangazo kwa soko la hisa la New York linaweza kutolewa kabla ya mwisho wa mwaka, ingawa msimu wa likizo unaweza kusababisha kusitishwa zaidi kwa sehemu hii ya mchakato kukamilika.

Lakini ingawa Ofisi ya Ratcliffe tayari inafanyia kazi mipango ya kurekebisha muundo wa soka wa United, vyanzo vimesema itachukua kati ya wiki nne hadi sita kwa Ligi Kuu England kuridhia mabadiliko ya mtindo wa umiliki wa klabu hiyo.

Kutokana na kipindi cha Krismasi na mwaka mpya, mchakato wa kuidhinisha huenda usianze hadi wiki ya kwanza ya Januari, na hivyo kuacha United ikikabiliwa na uwezekano wa dirisha la mwisho la uhamisho chini ya umiliki wa Glazer mwezi ujao.

Colette Roche, Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa United, aliambia kongamano la mashabiki wiki hii vikwazo vya kifedha vitaizuia klabu kufanya nyongeza muhimu kwenye kikosi cha Erik ten Hag katika dirisha la usajili la mwezi ujao.

Uhamisho wa mkopo unawezekana, lakini kwa United kuhitaji kuchangisha fedha, hakuna uwezekano mkubwa wa kuingia, hata kama makubaliano yatafikiwa ili kumtoa Jadon Sancho, ambaye hajahusishwa na kikosi cha kwanza tangu agombane na Ten Hag Septemba, mwaka huu.

## Mahadhi, Balama waondoka Coastal

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI Mapinduzi Balama na Juma Mahadhi, wameihama Coastal Union ya jijini, Tanga ambayo inatajwa iko katika hatua za mwisho za kumsajili straika wa Mbuni FC, Salim Aiyee.

Taarifa iliyotolewa na Coastal Union jana imesema uamuzi wa kuachana na nyota hao wa zamani wa Yanga umefikiwa kwa makubaliano na faida ya pande zote mbili.

"Balama, kwetu sisi ulikuwa zaidi ya mchezaji, nidhamu, weledi, uungwana na ubora wa kiwango chako ni vitu tutaendelea kuvikumbuka sana, wewe ni familia kwetu, tunakutakia lila la kheri katika changamoto mpya," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Klabu hiyo pia imempa mkono wa kwaheri Mahadhi ambaye ilimlea tangu akiwa kinda hadi mwaka 2016 aliposajiliwa na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga na baadaye kurejea Tanga.

"Tumevuka milima na mabonde pamoja, tumepitia machungu mengi, tumefurahia nyakati nzuri pamoja na wewe, kutoka kuwa nyota katika kikosi chetu cha vijana mpaka kuwa nyota katika timu yetu na nyingine ulizokwenda, karibu tena, Coastal Union ni timu yako, tunakutakia kila la kheri,"

## Wavu Z'bar waunda Kamati ya Mapinduzi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha Mpira za Wavu Zanzibar (ZAVA), kimeunda kamati maalumu itakayosimamia mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yatafanyika kuanzia mapema mwezi ujao, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa ZAVA, Kassim Haidar Jabir, alisema lengo la kuunda kamati ni kuongeza 'uzito' wa mashindano hayo ambayo yatasaidia kuibua na kuendeleza vipaji vya wachezaji wao.

Alisema kamati ya hiyo ya kusimamia mashindano ya wavu ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar itakakuwa na wajumbe tisa na itaongozwa na Mwenyekiti wake, Salum Kassim Ali.

Aliwataja wajumbe wengine wa kamati hiyo ni pamoja na Khamis Haji Msabah ambaye atakuwa Katibu, Mwajuma Juma, Ameir Msimu, Said Ali 'Raju', Mohammed Yussuf, Burhan Ali, Eutist Mwakanjuki na Mtumwa Rajab.

"Tumeunda kamati hii chini ya mwenyekiti mwenye uweledi mkubwa lakini alikuwa mchezaji mzuri wavu, kamati itaipa hadhi kubwa mashindano hasa ukizingatia ukubwa wa sherehe za miaka 60," alisema Haidar.

# BITEKO ASHIRIKI, APONGEZA UBUNIFU ROMBO MARATHON

**Na Mwandishi Wetu,** ROMBO

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ambaye alishiriki Rombo Marathon zilizofanyika mjini hapa jana amewapongeza waratibu kwa kuandaa ubunifu wa kuhifadhi mazingira na kuimarisha huduma za kijamii kupitia mbio hizo.

Mbio hizo zilihusisha umbali wa kilomita tano, kilomita 10 na kilometa 21, zinatarajia kuendelea kuimarika kila mwaka na kufikia malengo yake.

"Nimeelezwa lengo la Rombo Marathon ni kuhamasisha utunzaji wa mazingira, kukuza utalii wa ndani, kuchangia fedha kwa ajili ya shule za msingi na sekondari wilayani Rombo ili ziweze kuwa na vyoo salama na kupata fedha zitakazowezesha kupandisha hadhi ya hospitali ya Huruma iliyoko Wilayani Rombo ili iweze kuwa Hospitali ya Rufaa.

Niwapongeze sana wote kwa uratibu wa jambo hili lenye manufaa," alisema Biteko ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mbio hizo.

Aliongeza serikali itaendelea kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazofanywa na wananchi katika kujiletea maendeleo ikiwamo uanzishaji wa maeneo ya huduma za kijamii kama vile shule, vituo vya afya na michakato mingineyo.

Alisema licha ya Rombo Marathon kuchangia katika kuboresha huduma za kijamii, washiriki kutoka ndani na nje ya nchi pia wamepata fursa ya kubadilishana mawazo na uzoefu katika nyanja mbalimbali ikiwamo za kiuchumi na kijamii.

Alimpongeza Mbunge wa Rombo ambaye pia ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda kwa kuanzisha mbio hizo ambazo mwaka huu zimefanyika kwa mara ya pili huku akieleza ubunifu huo unapaswa kuigwa katika maeneo mengine nchini.

Pia Biteko amepongeza utamaduni wa watu wa Kilimanjaro ambao hurudi katika maeneo yao wakati wa sikukuu za mwisho wa mwaka na kueleza kurudi nyumbani kunasaidia kufahamu changamoto zilizopo na kuzitatua, ametoa wito kwa wananchi wa maeneo kuiga utamaduni huo.

Naye Mkenda alisema mbio hizo zitakuwa zinafanyika kila Desemba 23 zikiwa na malengo maalum ambayo ni chanya kwa jamii.

Mkenda alimshukuru Biteko kwa kuheshimu mbio hizo na kukubali kushiriki na kueleza ushiriki wake utakuza marathon hiyo na kuimarisha kutoka ngazi ya wilaya na kwenda kitaifa.

Kwa upande wa mbio za kilometa 21 wanawake, Sara Ramadhani aliibuka mshindi na kufuatiwa na Nathalie Elisante huku Neema Mswadi akishika nafasi ya tatu na wanaume namba moja ilichukuliwa na Chigale Giniki, Nestory Steven na Agustino Sule alishika nafasi ya tatu.




Washiriki wa mbio za Rombo Marathon wakijiandaa kukimbia katika mashindano yaliyofanyika katika Wilaya ya Rombo mkoani, Kilimanjaro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Maxime awa wa 10 kutimuliwa*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Kagera Sugar kutangaza kuachana na Mecky Maxime hapo juzi, uamuzi huo umefanya idadi ya makocha waliofukuzwa au kuondoka wenyewe katika timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kufikia 10.

Hii ina maana 'meli' ya Ligi Kuu Tanzania Bara tayari imeshaawacha makocha 10 'nchi kavu' huku sasa ikiingia katika raundi ya 14, imebakisha moja tu kumaliza mzunguko wa kwanza.

Kagera Sugar ilifikia uamuzi huo ikiwa imepita siku moja tu baada ya kupokea kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Azam FC, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Kilikuwa ni kipigo cha tatu mfululizo, kikianza na cha bao 1-0 dhidi ya Coastal Union, Desemba 9, mwaka huu na kufuatiwa na kichapo cha mabao 3-0 ilichokipata Desemba 15, mwaka huu kutoka kwa Simba.

Hadi anatimuliwa alikuwa ameiongoza Kagera Sugar katika mechi 13, ikishinda michezo mitatu, sare nne na kupoteza michezo sita, iko katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara yenye timu 16.

Makocha wengine walioachana na timu ni Hans Van Pluijm na Ernest Middendorp waliokuwa Singida Fountain Gate, Zuberi Katwila (Ihefu SC), Cedric Kaze, Denis Kitambi (Namungo), Mwinyi Zahera (Coastal Union), Roberto Oliveira (Simba), Habib Kondo (Mtibwa Sugar) na Hemed Suleiman 'Morocco' aliyekuwa Geita Gold.

Kati ya hao ni makocha wawili tu ndio wamepata kazi katika timu nyingine, Katwila akirejea Mtibwa Sugar na Kitambi amejiunga na Geita Gold.

# Michezo

Jumapili Desemba 24, 2023

Nipashe



## Varane atajwa kurejea Madrid

UKU. 21



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephanie Aziz Ki (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Tabora United, Nakibinge, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma jana usiku. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Taifa Stars kwenda mawindoni Algeria

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) itaondoka nchini na kuelekea Algeria kwa ajili ya kuweka kambi ili kujiandaa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), ambazo zitafanyika mapema mwakani huko Ivory Coast.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema wanaamini Algeria ni sehemu sahihi kwa Taifa Stars kuweka kambi na baadaye kuanza safari ya kuelekea Ivory Coast kupeperusha bendera ya taifa.

Ndimbo alisema sehemu ya wachezaji wa timu hiyo wataingia kambini mapema kwa ajili ya kuanza maandalizi ya mechi ya kirafiki ambayo utawakutanisha nyota wa Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars) dhidi ya wenyeji Zanzibar Heroes katika mechi ya kirafiki ya ufunguzi wa Uwanja wa Amaan.

"Tunaenda katika nchini ambayo tunaweza kufanya maandalizi mazuri kuelekea katika fainali hizo, malengo yetu ni kupa muda mzuri kocha (Adel Amrouche), kuandaa kikosi chake kwa utulivu mkubwa," alisema Ndimbo.

Kuhusu mechi ya kirafiki ya kimataifa kabla ya kuelekea Ivory Coast, ofisa huyo alisema bado mchakato wa kupata timu ya kukutana nayo haujakamilika na utakapokamilika itawekwa wazi.

"Kwa sasa sitaweza kuzungumzia mechi hiyo (dhidi ya Misri), kwa sababu bado haijatufikia, kama kutakuwa na mechi za kirafiki, tutaweka wazi kama ilivyo kwa mchezo wetu dhidi ya Zanzibar Heroes," alisema Ndimbo.

Taifa Stars iko katika Kundi F na itaanza kampeni za kuwania ubingwa wa Afrika Januari 17, mwakani kwa kucheza dhidi ya Morocco na Januari 21 itavaana na Zambia na itamaliza mechi zake za hatua ya makundi Januari 24 kwa kukabili Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Katika kuhakikisha inapata maandalizi mazuri, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inatarajia kufanya harambee ili kukusanya fedha itakayofanyika mapema mwakani.

# Yanga haikamatiki, Simba SC yabanwa

## ●●● Aziz Ki afikisha mabao 10 wakati mabingwa hao watetezi wakiikaribia...

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane,** DODOMA

WAKATI kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephanie Aziz Ki, ameendelea kuonyesha ubora wake baada ya kufunga bao pekee katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tabora United, Simba imelazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMC katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam, Complex Dar es Salaam jana.

Mabingwa hao watetezi jana walifikisha pointi 30 huku Aziz Ki akifikisha mabao 10 msimu huu na kuendelea kuongoza katika orodha ya wafungaji wa ligi hiyo.

Aziz Ki anafunga bao la tatu kwa mkwaju wa faulo, akizifunga pia JKT Tanzania na Azam FC katika mechi zilizopota.

Hata hivyo, kipa wa Tabora United, John Nobo, alifanya kazi ya ziada kwa kuokoa faulo nyingine zilizochezwa katika maeneo hayo hayo, mpigaji huyo huyo akipiga kwa staile ilele.

Yanga iliwachukua dakika 21 kupachika bao hilo, mfungaji akifunga kupitia mpira wa faulo aliyopiga nje kidogo ya eneo la 18 kwa kutumia mguu wake wa kushoto na mpia ulikwenda moja kwa moja nyavuni baada ya kumshinda Nobo kuokoa , aliyeruka bila mafanikio.

Kuingia kwa goli hilo kuliongeza kasi ya mchezo kwa wachezaji wa Yanga ambapo waliendelea kulisakama lango la wapinzani wao lakini umakini ulikuwa mdogo kwenye kumalizia mashambulizi yao.

Dakika sita kabla ya Yanga kupata bao, Max Nzengeli, alikosa goli la wazi baada ya mpira wake wa kichwa kupita kidogo juu ya lango la Tabora baada ya kuuganisha krosi nzuri iliyopigwa na Kibwana Shomari.

Tabora United walijitahidi kujibu na dakika ya 58 walikosa goli baada ya shuti lililopigwa na Najim Mussa, aliyekuwa nje kidogo ya eneo la hatari kuokolewa na kipa wa Yanga, Djgui Diarra, na 'kuzaa' kona tasa.

Makosa ya golikipa, Ayoub Lakred, yaliinyima Simba pointi tatu muhimu na kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMC katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana na kuendelea kusalia katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Ni matokeo yaliyojirudia kama mechi ya mzunguko wa kwanza msimu uliopita timu hizo zilipotoka sare kama hiyo mechi iliyochezwa Septemba 7, mwaka jana, Moses Phiri na Habib Kyombo wakifunga kwa upande wa Simba na Matheo Antony na George Makang'a wakiibeba KMC.

Wakati mashabiki wa Simba wakifikiri wangeondoka na ushindi, shuti la mbali lililopigwa na mtokea benchi, Tepsi Evans, lilitemwa na Lakred kwa nia ya kuupoza na kuudaka tena, lakini kwa bahati mbaya mpira ulikwenda mbele huku akiteleza na katika juhudi za kuuwahi, straika wa KMC, Waziri Junior, aliujaza wavuni kwa shuti kali, dakika mbili kabla ya mechi kumalizika, huku akiitanguliza timu yake kwa bao la kwanza dakika ya 30.

Hayakuwa matokeo mazuri kwa Simba iliyofikisha pointi 23 kwa michezo 10 iliyochezwa, ambapo ilitakiwa kushinda ili kuendelea kuzifukuza Yanga na Azam FC zilizo juu yake, huku pointi moja ya KMC imemwondoa katika nafasi ya tano mpaka ya nne, ikifikisha pointi 21.

Kipindi cha pili, Simba iliingia kwa nguvu, baada ya Mzamiru Yassin na Jean Baleke kuingia, ambapo ilifanya mashambulizi mengi na kufanikiwa kupata mabao mawili ya haraka haraka dakika ya 56 na 58.

Saido Ntibazonkiza alifunga bao la kusawazisha kwa penalti, baada ya Ibrahim Elius, kuunawa mpira wa krosi uliopigwa na Denis Kibu na dakika mbili baadaye, Baleke alifunga la pili akiunganisha krosi ya Kapombe, ambaye naye alikuwa ametangulizwa pande safi na Kibu, aliyehusika katika magoli yote mawili.

Linakuwa ni bao la nane kwa Mkongomani Baleke katika msimu huu akiwa sawa na Feisal Salum 'Fei Toto' wa Azam FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >